


# AMINI TU

 ...?...Mungu amewapa, kwa hiyo pamoja tunaweza kumtumikia Bwana Yesu. (Asante. Jambo ndilo hilo, ninii tu...)

<sup>2</sup> Loo, nina furaha sana leo, kwenye mahojiano ya faragha, jinsi Bwana alivyofanya mambo makuu, nami ninashukuru sana kulihusu. Na sasa, kesho usiku, uh, kesho ni Ijumaa, nilikuwa nikifikiri kesho ni Jumamosi. Hatutataka kusahau Kiamshakinywa cha Wafanyabiashara kitaandaliwa hapa, naamini katika shule hii. Nami nadhani, wao huwauzia tiketi, sivyo, ama kitu fulani? Nao, nadhani, kila mtu anaelewa jinsi tu unavyopata hi—hizo tiketi, na kadhalika, kwa ajili ya kiamshakinywa.

<sup>3</sup> Tungefurahi kama ungeweza kuja na kuona, uh, ukijisikia kuongozwa kuja. Sasa, Billy sikuzote huniambia, kasema, “Kuna jambo moja unalofanya, Baba, ni kuwachosha watu. Wamechoka kwa vyovyote vile,” kasema, “wameketi pale kwa saa nyingi. Unahubiri kwa muda mrefu *sana*.”

<sup>4</sup> Ndipo nikasema, “Vema, Mwanangu, nitajaribu kufidia hilo katika mkutano wa Chicago.” Nikasema, “Nitaweka saa yangu kwenye kila dakika ishirini, na ndipo itakapopiga kengele, nitaondoka papo hapa, na kuitisha mstari wa maombi.”

Naye akasema, “Afadhali usiweke, kwa sababu haitaninii...”

<sup>5</sup> Mnajua ililia mara mbili au tatu, hata ikajizima tu, kamwe sikujua. Ninapiga kelele nyingi sana hapa juu, mbona, hata si—sikuisikia wakati ilipolia, na kwa hiyo inanibidi tu, ninii tu, natumaini siwachoshi, mwajua, si—siji hapa kwa ajili ya jambo hilo. Na—naja, nami ninampenda Yeye sana, nami najua tuna mengi sana yanayopaswa kufanywa, moja kwa moja kwenye wakati huu, nami ninajaribu tu kushindilia mengi kupita kiasi katika usiku mmoja, mnaona, na bila kujua ni wakati gani ambapo tutaitwa tuondoke. Halafu basi nafikiri, vema, sijui ni wakati gani nitaitwa niondoke, wala hakuna mmoja wetu ajuaye hilo, na kwa hiyo afadhali basi tufanye tuwezavyo, wakati tunapoweza kulifanya.

<sup>6</sup> Nimemsikia mama yangu...Sijawahi kuwa kwenye dansi maishani mwangu, bali nilisikia...ila tu da—dansitakatifu wakati mmoja kanisani, kamwe sisahau hilo, wakati tulipokuwa tungali kanisa la Kibaptisti. Daima ningekosoa, kwa namna fulani, moyoni mwangu, nisingelisema kwa sauti kubwa, kwa sababu ni—ningeogopa kufanya hivyo, chochote afanyacho Mungu.

<sup>7</sup> Nilikuwa, sikuzote kwa namna fulani nilifikiri lilikuwa ni jambo la kigeni kuona, nilipoona, nilipofahamiana kwa mara ya kwanza na Wapentekoste, nikawaona wakicheza, mwajua, wakicheza dansi. Nikawaza, “Sasa, mnajua, hilo haliko katika Biblia.” Nikasema, “Vema, wanachezea nini dansi?”

<sup>8</sup> Ndipo usiku mmoja nilikuwa nikifundisha kutoka kwenye chati juu ya Danieli na Ufunuo, ulikuwa ni usiku wa Mwaka Mpya, nilikuwa nikitaka kufundisha kwa chati mpaka usiku wa manane, haikuwa ni chati, kitu kama ubao wa kuandikia, nilikuwa nikifundisha. Ba—basi kulikuwa na baadhi ya Wapentekoste waliokuwa wametoka Louisville. Walikuwa pamoja na, loo, dada kadhaa, dada mmoja aliyekuwa mchungaji wa kanisa moja kule naye alikuwa na, walikuwa na mbao za kufulia, na kastabini, na—na kila namna ya vitu vidogo vya kufanyia makelele, na—nao wote wakapatanisha kwa njia fulani, sijui ilikuwa ni nini, nao, basi msichana akaanza kucheza piano, na ndipo wasichana hawa wote huko juu wakaanza kugongagonga hizo mbao kwa kastabini na kadhalika.

<sup>9</sup> Na—nao wa—walipata, walikuwa wakiucheza ule wimbo, “Kutakuwako na mkutano hewani, hivi karibuni,” ama kitu fulani. Vema, maskini msichana huyo alikuwa akicheza, maskini mama mchungaji, akageuka tu mweupe, loo, kama tu chaki. Naye akaanza tu kuucheza hivi kwamba, sinini, sijawahi kuona kitu chochote kikicheza namna hiyo maishani mwangu. Ndipo nikawaza, “Sasa, ni kitu gani hicho?” Ndipo basi, mmoja kwenye huo ubao, akaanza kufanya jambo lile lile. Ndipo hapa, wawili au watatu wakasimama, kisha maskini mwenye kichwa kidogo cha rangi ya shaba kikaanza kucheza dansi moja kwa moja sakafuni, nikawaza, “Loo, jamani!”

<sup>10</sup> Moja kwa moja juu chini sakafuni, kwa nguvu alivyoweza kwenda, akicheza dansi tu, namna *hiyo*, maskini msichana mdogo, yapata umri wa miaka kumi na sita, kumi na minane. Mimi mwenyewe nilikuwa tu ni kijana. Nami, “Sasa, hilo si ni jambo fulani? Hapa hapa kanisani mwangu. Jinsi nitakavyowahi kuishia hilo!” Mnaona? Huku nikimwangalia namna hiyo. Ndipo nikawazia, “Kwa nini wanafanya hivyo? Kwa nini iwabidi kufanya hivyo? Kwa nini wasingeweza tu kupiga muziki wao na kuendelea na kuachana nayo, namna hiyo?” Nikawaza, “Vema, hilo ni baya sana.”

<sup>11</sup> Nikawaza, “Sasa, katika Biblia kuna kitu kama kucheza dansi?” Ndipo nikakumbuka ya kwamba Daudi alicheza kulizunguka lile sanduku, wakati alipoona hilo sanduku likija. Mnaona? Alicheza mbele za Bwana, naye Bwana akasema, “Yeye ni mtu anayependeza moyo Wangu.” Nikawaza, “Vema, sasa, hiyo ni...yeye...Kwa nini alicheza dansi?” Vema, walipata ushindi.

<sup>12</sup> Naye Miriamu, walipovuka Bahari ya Shamu, Musa aliimba

katika Roho, ndipo Miriamu akachukua tari, akaanza kuipiga, nao hao wakapanda juu, wakashuka ukingoni, binti wote wa Israeli, wakicheza katika Roho. Mnaona? Nami nikaona kumbe kucheza dansi ni wakati walipopata ushindi.

<sup>13</sup> Nikawaza, nikaanza kuwazia, “Vema, labda, sina ushindi, wa kutosha.” Mnaona? Nikaanza kuliwazia, nanyi mwajua, baada ya kitambo kidogo nikaanza kupigapiga mguu wangu, na kabla sijajua nilikuwa huko nje nikicheza dansi pamoja na msichana huyo, huko nje kwenye marefu ya kanisa.

<sup>14</sup> Loo, nilitiwa alama wakati huo. Ninaweza tu kuona mwonekano kwenye uso wa watu hao bado, wakimwona mchungaji wao huko sakafuni pamoja na huyu, maskini msichana huyo akicheza dansi kote, mimi huyu hapa huko, pia. Kamwe sikuwahi kuwa kwenye sakafu ya dansi maishani mwangu, bali ingenibidi kulighairi na kusema, “Ilikuwa kwenye *ile*,” lakini hiyo ilikuwa ni sakafu ya kanisa. Kwa hiyo wakati sisi . . .

<sup>15</sup> Mnajua, yote aliyo nayo ibilisi, a—a—aliyaiga kwa kitu *halisi* alichu nacho Mungu, hivyo tu, vivyo hivyo hasa. Ibilisi hawezi kuumba, yeye ni mpotoshaji tu wa kile kilichoumbwa, mnaona. Kwa hiyo hawezi kuumba, yeye si muumba, yeye ni mpotoshaji.

<sup>16</sup> Udhalimu ni—ni nini? Ni haki iliyopotoshwa. Mnaona? Ni halali kwa mwanamume kumchukua mke, na—na awe mu—mume kwake katika uhusiano wa kifamilia. Lakini mwanamke yuyo huyo, uh, mwanamke mwingine kwenye tendo lile lile, linamhukumu, na kuipeleka mbali nafsi yake, mnaona, ni kosa. Ni kitu gani? Haki iliyopotoshwa. Mnaona? Na ni ninii . . .

<sup>17</sup> Ukweli daima ni sahihi. Uongo ni nini? Ni ukweli uliyopotoshwa, mnaona, hufanya uongo. Kwa hiyo hivyo ndivyo dhambi yote ilivyo, ni haki iliyopotoshwa.

<sup>18</sup> Kwa hiyo nilipokuwa nikimsikia mama yangu akisema, alikuwa akienda kwenye dansi za kale, yeye na Baba kwenye namna hiyo ya ninii, mnaona, hao, walikuwa na fidla ya kale wangekuja, wasimame pembeni na kucheza fidla na hao watu wa Kentucky, naye Baba, yeye hakuwa na pesa zozote, mwajua, mnapaswa kuwa na pesa kidogo za kuchezea mifukoni mwenu, nami nikamwona akienda kwenye birika, anachukua misumari michache, anaiweka mifukoni mwake, mwajua, naye angecheza kote, yeye na Mama, nao wangeshinda zawadi. Ninaweza kumwona akivuta sketi yake juu *hivi*, mwajua, na hiyo dansi ya kurukaruka, mwajua, moja kwa moja karibu, kuzungukana namna hiyo. Nami ningemwona Baba, nikawazia, “Hilo ni—hilo ni baya Baba, hiyo misumari, hiyo si pesa,” mnaona. Nilijua hakuwa na pesa zozote, alikuwa na misumari michache mfukoni mwake, ikigongagonga juu chini namna hiyo, mnaona.

<sup>19</sup> Nao wangepanya hivyo moja kwa moja mpaka kwenye mapambazuko. Na baadhi ya watu waliondoka nyumbani,

ninii. . . Loo, ninii, loo, watu wa Kentucky wangekuja huku, nao wangecheza dansi nyumba kwa nyumba. Halafu basi, wangeenda nyumbani asubuhi moja, wamebeba viatu vyao mikononi mwao, maana miguu yao ilikuwa inauma sana kwa kucheza dansi.

<sup>20</sup> Vema, kama unaweza kufanya hivyo kwa ajili ya ibilisi, basi kwa nini usikae, na kutuacha tuhubiri usiku kucha, na kumsifu tu Mungu, na—na kuingia katika Roho, na, mnaona? Hakika. Kama hiyo—kama hiyo ni kwa ajili ya utengano wa Milele, vipi kuhusu Uzima wa Milele? Hebu. . . Tunaweza kuithamini *hii* vile vile, zaidi ya vile tunavyopaswa kuthamini *ile*, bila shaka. Lakini Shetani angetuchosha kwa jambo hili, upesi sana, ama kutwambia tulikuwa tumechoka sana. Lakini nawaambieni, amekuwa na wakati mgumu sana nami, kunichosha kwake.

<sup>21</sup> Ninakumbuka wakati nilipoonywa ugonjwa wa tumbo, yeye, Shetani alisema, “Mbona, afadhali usile,” kasema, “kwa sababu daktari alisema ukila, utakufa. Ulikuwa na tumbo lenye vidonda, na kasema ni kidonda kimoja tu kikubwa, kilichojaa damu.”

<sup>22</sup> Lakini Bwana alisema Yeye aliniponya, kwa hiyo ilinibidi kuamini neno la mtu fulani, kwa hiyo ni—nikaliamini Neno la Mungu. Na kwa hiyo, loo, karibu iniunguze! Nilikuwa tu, maji ya moto yakitoka kinywani mwangu, na kwa hiyo, siku mbili ama tatu, nilikuwa nikipigwa Kwake, niliponywa, kwa hiyo hilo ni, hilo namna *hii*.

Kasema, “Unajisikiaje, Bw. Branham?”

Nikasema, “Loo, najisikia vizuri,” nikikanyaga tu namna hiyo.

<sup>23</sup> Mtu fulani akasema, “Ulisema uongo.” Mimi sikusema uongo, nilikuwa nikikiri. *Kukiri* maana yake ni, “sema jambo lile lile.” Kwa kupigwa Kwake, niliponywa, kwa hiyo hilo ni, hilo latosha, mnaona. Nilikuwa nikikiri.

Na kwa hiyo, Shetani akaniambia, kasema, “Unaleta aibu.”

<sup>24</sup> Nikasema, “Sasa, angalia hapa, maskini wee, kama—kama unafurahia kunisikia nikishuhudia, wewe simama huku, lakini kama hufurahii, afadhali uondoke, maana ni—nitashuhudia kwa vyovyote vile.” Basi jambo ndilo hilo, inakubidi tu kumjulisha umesimama upande gani, kisha uchukue msimamo wako, na halafu usimame.

<sup>25</sup> Na hivyo ndivyo tu inavyotupasa kufanya daima, ni kufikia mahali tunapojua ya kwamba tuko sahihi, ndipo basi unaamini hilo, huwezi kuwa na imani isipokuwa unajua uko sahihi. Usijaribu kufanya hivyo ili kumdanganya, sasa, hatakubali udanganyifu wako. Unaona? Usimdanganye. Lakini unapoliamini kweli, hudanganyi basi, kitu fulani tayari kimekushuhudia, na basi wewe—basi uko sahihi.

26 Sijali, huenda usininii, hakuna mtu aliyepata kukuwekea mikono, huenda usihisi chochote kamwe, bali maadamu kitu fulani kimethibitisha moyoni mwako ya kwamba ni Neno la Mungu na mapenzi ya Mungu kwako, hilo tu ndilo linalohitajika. Na mara nyingi, karama hizi na kadhalika, zinatia moyo tu.

27 Ninamwangalia mhubiri Mbaptisti aliyeketi hapa mbele yangu, usiku wa leo. Kama sijakosea, je, huyu ni Bw. Daulton, aliyeketi hapa, kutoka Somerset, Kentucky? Nilidhani ndiye. Ninamkumbuka Ndugu Ed Daulton. Loo, jamani! Mbaptisti, vema. Naye alipanda akaja, na, bali aliamini, kisha akaja kanisani, na kumpokea Roho Mtakatifu, ndipo akashuka akarudi. Na bila shaka, ujirani wake wote ulimsikitisha, kama kawaida. Na kwa hiyo, basi wakati Roho Mtakatifu alipokuwa ameeleza juu ya, yale tunayotazamia kutukia wakati wowote sasa, karama nyingine ambayo itaongezewa kanisa, na ni jambo la ajabu.

28 Nasi tumeninii. . . Labda mmesoma makala katika magazeti yetu ya kidini kuhusu jambo hilo, kuhusu kuchakulo, na kadhalika. Basi Ndugu Daulton alikuwa na watoto wawili. Vema, nafikiri, ni wangapi? Yapata watoto wanane, nafikiri ni. . . ? Watoto tisa, watoto tisa, na matineja, nanyi mnajua jinsi walivyo, kwa namna fulani. . . Na maskini baba na mama, jinsi walivyoomba kwa bidii sana, kwamba Mungu awaokoe watoto wao.

29 Siku moja maskanini. . . Alikuwa amemwona Roho Mtakatifu akizungumza na mwanamke fulani na kumwambia, “Omba tu utakalo, sasa hivi, na Mungu aliniambia nikupe.”

Kasema, “Niombe nini?”

30 Nikasema, “Vema, una dada mlemavu aliyeketi hapa, ambaye amekuwa mlemavu tangu kuzaliwa.” Na kuna mtu aliyeketi hapa, usiku wa leo, Banks Wood, ambaye alikuwa ameketi moja kwa moja pamoja nami, jina la mwanamke huyo ni Bibi Wright. Nami nikasema, “Una baba na mama wazee; unaishi kwa chini ya dola mia mbili kwa mwaka kwenye maskini shamba hilo duni, kule, mwanamke mjane.” Nikasema, “Kuna mambo mengi ungeweza kuomba, Dada Hattie, lakini,” nikasema, “Mungu yeye yule aliyeniambia kuhusu kuchakulo hao wakati nilipozungumza, kuchakulo hao walikuwa wamesimama pale pale,” na kufanya hivyo mara saba mfululizo, nikisimama pale pale, ambapo unaangalia na kuliona, ambapo ilikuwa haiwezekani kabisa kwa mmoja kuwa ameketi ukutani *pale*, ikithibitisha tu jambo fulani, halafu nikasema, “Yeye anianiambia nikwambie uombe utakalo. Alisema ungeomba, nipate kulisema.”

Akasema, “Vema, nise me nini?”

Nikasema, “Omba lolote utakalo, utapewa papa hapa. Kama sivyo, basi ni—nimesema uongo.”

<sup>31</sup> Naye akasema, “Vema,” kasema, “Sijui niombe nini, Ndugu Branham,” akasema. Alikuwa na wavulana wawili matineja, na nena juu ya waasi, walikuwa hivyo, na kwa hiyo, wakimhuzunisha tu wakati wote, maskini mama mjane. Na kwa hiyo, mumewe, nilimwoza kwa mumewe. Nao walikuwa. . . Mumewe alikuwa ameuliwa na trekta. Nao hao wavulana walikuwa tu wameingia wazimu. Ndipo akasema, “Vema, wokovu wa wavulana wangu wawili.”

Nikasema, “Ninakupa hao wavulana wawili katika Jina la Yesu Kristo.” Ndipo wote wawili wakaanguka pajani mwake, wakamjia Kristo.

<sup>32</sup> Sasa, Ndugu Banks Wood yuko mahali fulani ameketi hapa katika jengo hili, usiku wa leo, ambaye alikuwepo kuona jambo hilo likitukia. Wavulana wote wawili wako sawa, walishiriki Kutawadhana miguu wakati wote, Ushirika kanisani. Na wakati tunaposhiriki Kutawadhana miguu, wale wanaotawadhana miguu, tunaweka mikono yetu juu yao na kuomba. Maskini jamaa huyo hivi majuzi usiku, yapata umri wa miaka kumi na minne, mchungaji wetu, Ndugu Neville, alikuwa ameweka mikono yake juu yake, akimwomba, maskini mtoto anayependeza sana.

<sup>33</sup> Kwa hiyo Ndugu Ed Daulton akaona hilo likitukia, alikuwa akiwaomba watoto wake, akatoka nje, naye akageuka, ndipo Roho Mtakatifu akasema, “Nena kwa ajili ya watoto wa Ed.”

<sup>34</sup> Nami nikasema, “Ndugu Daulton, Roho Mtakatifu aniambia kwa karama iyo hiyo ambayo tunatazamia kudhihirishwa kikamilifu hivi karibuni, ninakupa watoto wako katika Jina la Yesu Kristo.” Basi alipofika nyumbani kule, binti yake na wanawe, tayari wameitoa mioyo yao kwa Kristo. Maili chache tu chini huko nchini kutoka kwangu.

<sup>35</sup> Nami nafikiri kila mmoja wa watoto wako ameokoka na kujazwa na Roho Mtakatifu na yuko tayari. Hiyo ni kweli, Ndugu Daulton? Kuna yeyote kati yao aliye pamoja nawe? Binti mmoja. Je, huyo ndiye aliyeokoka mara moja? Binti wa kwanza aliokoka kesho yake asubuhi. Na kila mmoja wa watoto wake sasa ameokoka. Jinsi, Roho Mtakatifu, Mungu anaposema jambo lolote, Yeye hutimiza Neno Lake, ni hivyo tu! Mnaona?

<sup>36</sup> Sasa, ningewezaje kuwaokoa watoto hao? Mnaona? Si—sivyo, kama si maneno yako mwenyewe, kama si mawazo yako mwenyewe, basi daima ni—ni ya kile kinachokuvuvia. Na kama ni Mungu, basi ni Neno la Mungu, mnaona. Kwa hiyo hivyo ndivyo ilivyo, kwe—kwenye mikutano hapa usiku, unapoono mambo hayo yakitukia, huyo si mimi, nisingeweza kufanya hivyo, ni Mungu anayefanya hivyo. Na kama utaamini tu, basi hilo tu ndilo unalopaswa kufanya, ni ku—kuamini tu.

<sup>37</sup> Sasa, vema, wakati umekaribia, itisha mstari wa maombi, Billy. Kwa hiyo, ninachukua tu wakati mwingi sana. Lakini

mwajua, ninataka ku—nataka kufanya miadi na watu wote karibu na Chicago hapa.

<sup>38</sup> Naye huyu—huyu ndugu anayeimba hapa usiku, Ndugu Melvin, jinsi ninavyopenda kumsikia mvulana huyo akiimba! Na—nataka kumsikia akiimba, *Nikumbuke*, moja ya siku hizi usiku kabla sijaondoka. Halafu kuna dada mweusi anayeimba kwenye Wafanyabiashara Wakristo. Loo, jamani, u—unapaswa kumsikia akiimba *Merikebu Hoyee!* Nami nilimwambia mke wangu, ameketi pale nyuma, usiku wa leo, basi ni—nikamwambia, natumaini atamsikia mama huyo akiimba *Merikebu Hoyee*, na Ndugu Melvin akiimba, “Nikumbuke wakati machozi yakitiririka chini.” Loo, jamani, hakika natumaini tutapata haya.

<sup>39</sup> Na kuna ndugu mdogo kule kwenye mkutano huo hivi majuzi asubuhi, ameketi hapa nyuma mahali fulani. Nilitikisa ninii wake. . . *Huyu* hapa, yeye na mke wake. Jamani, nena kuhusu kuimba! Basi mtakapofika Utukufuni, nami na—natamani. . . Sikuzote nilitaka kuimba, afadhali niimbe kuliko kuhubiri wakati wowote. Kwa hiyo, na—napenda kuimba vizuri sana, kwa hiyo daima nilisema, “Waimbaji wote mashuhuri wa dunia watakusanyika Kule wakiziimba hadithi, jinsi walivyoshinda, huko kwenye ubavu wa kilima kikubwa Utukufuni, kuvuka tu Mto wa Uzima, ng’ambo ya pili, ninataka kuketi na kuwasikiliza.”

<sup>40</sup> Kwa hiyo ninataka kuwaalikeneni ninyi nyote watu wa Chicago kukutana nami kule, sasa, na—na—nasi tutaketi chini, tuwasikilize wakiimba, kwa hiyo hatutakuwa na ninii yoyote. . . haitatubidi kuharakisha, na kuona kama watoto wataumia, ama chochote kile, watakuwa kule pamoja nasi, na hakutakuwa na chochote cha kudhuru wala kuangamiza. Nasi tutakuwa na wakati mwingi sana basi, na tutaongea tu kwa muda *mrefu* sana, tutakuwa tu na wakati mwingi wa kuongea.

<sup>41</sup> Sasa, nina Maandiko kadhaa ninayotaka kuyarejea, ninayo mengine yaliyoandikwa hapa katika kurasa fulani hapa. Nami ninataka kuanza, usiku wa leo, na kusoma, kwanza, Maandiko yanayopatikana katika Luka Mtakatifu 8:50, kwa ajili ya so—somo. Nalo somo langu, usiku wa leo, ni wimbo mrejeo walioimba kabla tu sijaingia: *Amini Tu*. Na Luka Mtakatifu mlango wa 8 na kifungu cha 50:

*Lakini Yesu aliposikia hayo, alimjibu, akamwambia,  
Usiwe na hofu, amini tu, naye ataponywa.*

Na tuinamishe vichwa vyetu, kwa muda kidogo tu, kwa ajili ya maombi.

<sup>42</sup> Mungu mwenye rehema, uliyemfufua tena Bwana Yesu, Mwanao, kutoka kwa wafu, na umemleta kwetu baada ya miaka elfu mbili, tunamwona siku baada ya siku, na usiku baada ya usiku katika mwili Wake usioonekana ukitenda kazi katika

Mwili unaonekana wa Kanisa Lake, akitimiza Maneno Yake. Na kama tulivyokuwa tukizungumza hivi majuzi usiku, Wewe uko kwenye ratiba kabisa, kila kitu kinaingia sawasawa kabisa, saa kuu ya wakati wa Mungu inapiga, kwa wakati ufaao. Ndipo, usiku wa leo, tunapona ya kwamba pigo hilo la mwisho la usiku wa manane liko karibu kupiga, Ee Yehova Mungu Mkuu, uturehemu.

<sup>43</sup> Na kama ninavyowazia usiku wa leo, hapa mbele yangu, nikiwashikilia walionunuliwa kwa Damu Yako, usikivu wao kwa dakika thelathini ama arobaini zifuatazo, “Niseme nini, Ee Mungu?” Maneno haya machache ambayo yametayarishwa yasingetosha, Bwana, bila upako Wako. Kwa hiyo ninaomba ya kwamba utayatia mafuta haya Maneno, usiku wa leo, ya somo hili, na jalia yapate mahali Pake pa kutulia, na kutupatia kile tunachohitaji tupate kujiandaa kwa ajili ya saa hiyo ambayo Yesu atakuja. Kwa sababu Mungu, niliona, huku macho yangu yamefunguliwa, dakika chache zilizopita, hiki hapa mbele yangu ni kile kitabu cha Wafanyabiashara Wakristo, ambamo Ndugu yetu wa thamani Tommy Nickel alitafsiri kutoka kwenye kanda ile ono lile, ama chochote kilichokuwa, Bwana, umeniruhusu kuona ng’ambo ya pazia kule, na Ee Mungu, nikasema, “Laiti ningaliweza tu kurudi nyuma kwa ajili ya . . . Ni—ningeshawishi, ningewasihi watu. Loo, hawapaswi kukosa Hilo, Bwana.”

<sup>44</sup> Kuna watu hapa ambao wamegawa riziki zao pamoja nami, kwa ajili yangu na watoto wangu, na kati yao na watoto wao. Ninaomba, Mungu, ya kwamba *kwa njia moja ama nyingine*, jambo fulani linaweza kusemwa usiku wa leo, ambalo litaninii, tupate kumgawa Kristo miongoni mwetu usiku wa leo, apate kuwa Mwokozi wa kila mmoja wetu, na Mponyaji wa kila mmoja wetu, na Mfalme wetu ajaye. Ndipo tumaini hilo, liachwe hapa mioyoni mwetu. Jalia tuishi Milele pamoja Naye, katika ile Nchi isiyo na maradhi.

<sup>45</sup> Ninaweza kuwawazia hao wanawake, jinsi walivyokuwa wakati mmoja, nikitambua hawa hapa wanawake wakongwe, wenye umri wa miaka tisini, nao hao huko, warembo na vijana. Na hao wanaume walio na mvi hapa duniani, hao huko, vijana na katika ujana wao Milele. Mungu, tusingeweza kukosa jambo Hilo.

<sup>46</sup> Tujalie, Bwana, usiku wa leo, ya kwamba kila mtu atachukua msimamo mpya usiku wa leo. Wabariki watakatifu na uwaponye wagonjwa, kwa kuwa tunajikabidhi, pamoja na somo hili, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya utukufu Wako. Amina.

<sup>47</sup> Yesu alikuwa ndiyo kwanza amekataliwa kutoka kwenye uamsho mkuu. Yeye daima alikuwa katika shughuli za Baba; na—napenda hilo. Sisi. . . Mimi, mwenyewe, nina muda mwingi sana ambao na—nafikiri na—nautumia kijinga, nasi sote



tunajisikia hivyo. Nasi tunasongwa sana hata inatubidi kwenda mahali fulani na kujituliza.

<sup>48</sup> Lakini tulimwona Yesu daima katika shughuli za Baba; ninapenda hilo. Na hivyo ndivyo tunavyopaswa kuwa, hatupaswi kamwe kuwa wavivu katika wakati wetu. Wakati tulio nao, hatuna budi kuutumia kwa ninii, na—na kuuhifadhi wakati, kuukomboa, kwa sababu ni wa thamani, kila wakati tunapopata nafasi ya kumtumikia Yesu, tufanye hivyo, kila wakati tunaopata ili kumfanyia Mungu jambo fulani, tufanye hivyo. Fanya jambo fulani kwa ajili ya Kanisa na kwa ajili ya kuwaendeleza watu. Watu wengi, hivyo ndivyo tunavyopata kujua mambo haya ni kwa yale mtu fulani alituambia.

<sup>49</sup> Naye Yesu alikuwa ameondoka Galilaya, katika nchi aliyotoka, na kuvuka bahari, akijisikia kuongozwa, hapana shaka, kwenda huko Gadara kwa ajili ya uamsho. Hapana shaka, ila kwamba Baba alikuwa amemwongoza kuvuka bahari kwenda Gadara. Nanyi, sote tunajua hadithi ya kwamba kulikuwa na mtu mmoja tu aliyeokoka, huyo alikuwa ni mwendawazimu, huko Gadara. Naye alikuwa huko nje kondeni makaburini, alikuwa ameingia wazimu. Nao wakamfunga minyororo, nazo nguvu za pepo zingeweza kuivunja hiyo minyororo.

<sup>50</sup> Na—na mara nyingi nimewazia, nikizunguka kwenye hospitali za wendawazimu, na kumwalia mtu ambaye amepagawa na hizo nguvu chafu, jinsi walivyo na nguvu! Wanamchukua polisi, wakati mwingine, kuwadhibiti.

<sup>51</sup> Nakumbuka huko Florida, usiku mmoja m—mtu ambaye asingekuwa na uzito wa zaidi ya ratili mia moja na ishirini, aliwacha polisi watano kwa urahisi tu kama vile ungemcharaza mtoto wako. Ndi—ndipo basi huyo pepo mchafu alipomtoka, mbona, karibu alikuwa ni *bure*, yeye, mpole tu alivyoweza kuwa, bali ilikuwa ni pepo mchafu.

<sup>52</sup> Nami nikawazia, “Kama mtu aliyepagawa na pepo mchafu angeweza kuvunja minyororo, angefanya nini kama angekuwa amejisalimisha kabisa kwa Mungu, huku nguvu za Mungu zikimdhhibiti hivyo?” Angeweza kunyoosha kila mguu uliolemaa, na kufanya mambo makuu, kama angeweza tu kutiwa mafuta *hivyo* na nguvu za Mungu, kadiri ibilisi angeweza kumnyakua kabisa.

<sup>53</sup> Hivi mliona, ibilisi huo alikuwa amemnyakua mtu huyo kabisa, hata a—alimkiri Yesu? Kasema, “Tunajua Wewe ni Nani, Mtakatifu wa Mungu. Kwa nini unakuja kututesa kabla wakati wetu haujatimia?” Mnaona? Alikuwa amejisalimisha kabisa kwa ibilisi, mpaka ibilisi angeweza kutumia ulimi wake.

<sup>54</sup> Nanyi mwajua, napenda hilo. Natumaini hili halimwudhi mtu yeyote, bali tunaweza kujisalimisha kabisa kwa Mungu hata anaweza kutumia ulimi wetu, pia, ku—kunena katika lugha

zingine, na kuhubiri Injili, kuimba Injili, kunena maono ambayo tunayatazama, na siri za Mungu, kama tukijisalimisha tu kabisa kwa nguvu za Mungu, hivyo tu. Na iwapo ibilisi anaweza kumweka mtu chini ya mamlaka yake, na kufanya hivyo, Mungu anaweza kufanya nini na mtu, akimweka mtu chini ya mamlaka Yake? Mnaona? Kwa hiyo mwendawazimu huyu. . .

<sup>55</sup> Nanyi mnaona, wakati Yesu alipokuwa akivuka bahari, ibilisi alijua ya kwamba alikuwa njiani kuelekea kwenye ushindi mkuu, kumletea Mungu ushindi mkuu, naye akajaribu kumzamisha usiku huo, akasababisha dhoruba kutokea, na, bali Yesu alijua ya kwamba Mungu alikuwa amemtuma, kwa sababu Yeye alifanya tu yale Mungu aliyomwongoza kufanya.

<sup>56</sup> Hilo si lingekuwa zuri kama tungekuwa na ushuhuda kama huo, ndugu? “Nafanya tu yale yanayompendeza Mungu.” Hilo si lingekuwa zuri sana? Kama vile Henoko, alivyotembea na Mungu miaka mia tano na akawa na ushuhuda ya kwamba alimpendeza Mungu. Haikumbidi kufa, alipaa tu juu.

<sup>57</sup> Kwa hiyo basi, matembezi madogo ya alasiri, alianza tu kutoka nje, na kuwazia tu, “Vema, nimekuwa duniani muda mrefu vya kutosha, nitaendelea tu kupanda juu.” Ndipo akaanza tu, kwa imani, akawazia, “Vema, nimekuwa hapa muda mrefu vya kutosha, kwa hiyo kidogo nimechoka kuwa hapa, nafikiri nitaendelea tu kupaa juu mpaka nitakapofika kwenye Njia ya Kilimia Cheupe na kuendelea tu kupanda juu, nikabishe kwenye ule mlango.” Kwa hiyo hivyo ndivyo alivyofanya. Mnaona? Kwa imani alifanya hivyo, Biblia ilisema hivyo. Mnaona, alichoka tu kukaa hapa, akasema, “Vema, nitatembea tu niende Nyumbani, Mungu.” Akaenda tu juu kupitia hewani akitembea. Alifanya hivyo kwa imani, Biblia ilisema alifanya hivyo.

<sup>58</sup> Na kwa hiyo, loo, mimi—mimi, ninapohisi mauti yakija mlangoni pangu, na—nataka kuwa na imani ya namna hiyo, nanyi je? Niseme tu, “Vema, kwaheri ewe ulimwengu wa kale, nitakuacha sasa.” Na nianze tu kutembea. Niendelea tu kutembea nikipanda juu, na kuupita mwezi na nyota na kufika kwenye Njia ya Kilimia Cheupe, na kuingia kwenye sayari, na sayari, na nje ya sayari, na kuendelea tu niingie Utukufuni, hiyo ni kweli.

<sup>59</sup> Ndipo basi, tunaona ya kwamba ibilisi hawezi kumwanganiza mtumishi wa Mungu maadamu yuko katika mapenzi ya Mungu. Ndivyo alivyo, tunamwona akiinuka usiku huo, na ibilisi amekasirika sana, na atajaribu kumzamisha huko nje baharini, akasimama, Naye akasema, “Mbona mmekuwa waoga sana? Mnafikiri ningekuwa nikifanya lolote isipokuwa lilikuwa katika mapenzi ya Mungu? Mbona mnaogopa hivi?” Mnaona? “Mnahofu nini, hata hivyo? Mbona mmefadhaika hivi?”

60 Hilo ndilo jambo lile lile Yeye angetuambia usiku wa leo, ndugu, nadhani. “Mbona mnaogopa hivi?” Mnaona? “Kuna nini? Hivi mnaogopa kuniamini Mimi?”

61 Akasema, “Amani, tulia.” Nazo pepo na mawimbi yakamtii, wakavuka bahari. Loo, ni nzuri jinsi gani! Huyo hapo akavuka ng’ambo ya pili, ndipo mwendawazimu huyu akakutana Naye, na—na alipokutana naye, alitaka kumrarua vipande-vipande. Ndipo ibilisi akagundua ya kwamba Huyo alikuwa kidogo ni zaidi ya mwanadamu anayekuja, akitembea kule pamoja na hao watu wengine kumi na wawili.

62 Ndipo basi, alipomkiri Yeye kuwa ni Mwana wa Mungu, na kukiri ya kwamba yeye, mateso yake ya usoni, Yesu alisema, “Nyamazeni, lakini tokeni ndani yake.” Naye akamkomboa mtu huyo na majeshi hayo ya pepo. Nao pepo hao wakaenda kule na wakapata. . . Kama hawamo mwilini, wana—wanaonekana kuwa wasiojiweza. Kwa hiyo wakaenda kule na kuingia kwenye kundi la nguruwe kisha wakashuka, nguruwe elfu mbili, wakazama baharini.

63 Basi mwajua nini? Yesu alikuja kufanya uamsho, lakini wakati watu hao walipotambua itawagharimu nguruwe elfu mbili, hawakutaka huo uamsho. Kwa hiyo kama utawagharimu chochote, hawataki uhusiano wowote nao. Basi hiyo—hivyo karibu ndivyo ilivyo siku hizi, mwajua, Kama itakugharimu saa chache za usingizi ama—ama *chochote kile*, watu hawataki uhusiano wowote nao, mwajua.

64 Na kwa hiyo wakasema. . . Vema, wa—wao. . . Badala ya kuwa na uamsho, walitoka, watu wa mji huo, na kusema, “Ondoka nchini mwetu. Sisi kamwe. . . Hatukutaki hapa, ondoka tu. Sisi. . .”

65 Na, mwajua, ndipo Yesu akaangalia kote kwa mtu huyo aliyekuwa na akili timamu, na alikuwa amevaa nguo. Na kama. . . Mwajua, daima niliwazia pale, a—afadhali nisiingilie hilo, kama—kama, mnaona, mtu huyo, alianza *kuvaa* nguo alipokutana na Yesu, basi imekuwaje, tunadai tunamjua Yeye, na huku tunazivua wakati wote? Kwa hiyo kuna ninii. . . Na hiyo ni. . .

66 Wanasema tuna kichaa kwa kuhubiri mambo kama hayo, lakini sijui, mtu aliyekuwa. . . aliyekuwa uchi ndiye aliyekuwa mwendawazimu, kulingana na Biblia, kwa hiyo, basi alipomwona Yesu, alienda akavaa nguo zake tena. Kwa hiyo—kwa hiyo tunaona ya kwamba. . .

67 Mara nyingi nimeshangaa, nitakapofika Mbinguni, ninataka kumwona mtu huyo, nami ni—ninataka kwenda kule. . . Yesu asingemruhusu amfuata, Yeye alisema, “Rudi ukawaonyeshe watu kule yaliyokupata.” Nami nashangaa tu ushuhuda wake ulikuwa na—na uzito gani juu ya ufugaji wa nguruwe katika nchi

hiyo baada ya hapo. Si—sijui tu ushuhuda wake ulikuwa na nini, ulikuwa na uzito gani kule.

<sup>68</sup> Lakini hawakumtaka. Kwa hiyo nitasema jambo moja: Kama humtaki, Yeye hatakuchosha kwa nafsi Yake. La, la, Yeye hatajikusumiza Mwenyewe kwako, kamwe hakufanya hivyo. Yeye hubisha, wewe uko ndani, wewe ndiwe unayefungua mlango. Lakini Yeye atabisha, atakupa nafasi.

<sup>69</sup> Kwa hiyo basi, loo, walisema, “Hatukutaki. Sijali unaweza kuwakomboa wangapi, na jinsi gani, na nini, ni nani aliyekutuma hapa. Kama Mungu alikutuma hapa, nini basi? Kamwe hatutaki upuuzi wowote wa namna hiyo uende hapa karibu na kwetu. Unawafanya watu wetu wachanganyikiwe kabisa, kwa hiyo wewe rudi tu mahali pako.”

Akasema, “Vema.” Papo hapo Yeye akarundi, akaingia chomboni.

<sup>70</sup> Hapana shaka ilikuwa yapata saa nne asubuhi. Maskini Ndugu yetu Yairo, alikuwa—alikuwa ni mwaminio. Yeye—yeye, kwa kweli alikuwa ni mwaminio, bali kwa namna fulani alikuwa mwaminio wa siri. Na, mwajua, tuna wengi sana wa hao huku nje katika makanisa haya ya Methodisti, Baptisti, na Presbiteri. Kweli wanaamini ujumbe huu wa Pentekoste, wanaamini, bali kamwe hawawezi kufanya hivyo kwa sababu ya kanisa lao.

<sup>71</sup> Kwa hiyo Yairo akasema. . . Alikuwa ni mwaminio wa siri, kwa nje alikuwa amejunga na kundi la wasioamini. Na kwa hiyo, hivyo ndivyo walivyo watu wengi wazuri usiku wa leo, wameungana na wasioamini. Nayo Biblia ilisema, “Msifungiwe nira pamoja kwa jinsi isivyo sawasawa.” Usijifunge nira miongoni mwa wasioamini. “Ondokeni miongoni mwa wasioamini, mkajitenge, asema Mungu, nami nitawapokea, msiguse vitu vyao vilivyo vichafu. Nami nitakuwa Mungu kwenu, nanyi mtakuwa wana na binti Kwangu.”

<sup>72</sup> Kwa hiyo Yairo, hata hivyo, alikuwa kama wengi wa siku hizi, alikuwa amejifunga nira katika madhehebu, hata kwa kweli asingeweza kujiondoa kwake, kwa sababu alikuwa na jina mashuhuri, labda. Hebu tumwite, Dk. Yairo. Mnaona? Alikuwa ni . . . alikuwa na jina kuu la *Daktari*, labda, nyuma yake. Alikuwa ni kuhani, naye alikuwa—alikuwa mchungaji wa sinagogi kubwa. Lakini moyoni mwake angemfuata Yesu wa Nazareti, alikuwa ameiona hiyo miujiza. Angeenda nyumbani na kusoma, na kuangalia kote katika Maandiko, naye angesema, “Hiyo ni kweli kabisa!”

<sup>73</sup> Hebu tuwazie alikuwa amesimama pale siku hiyo wakati Simoni alipokuja. Alishuka kwenda kumsikiliza Yohana akihubiri, naye akasikia kuhusu, akawasikia wakimtangaza Yesu, na kuona Nuru hii ikishuka juu Yake pale, na kutulia juu Yake. Nasi tuliona Nuru iyo hiyo iliyokuwa juu Yake, ikimwambia maskini mvuvi huyo, “Mbona, jina lako ni

Simoni, nawe ni mwana wa Yona.” Labda, mwajua, baba yake alikuwa... huenda alikuwa mfuasi wa sinagogi la mtu huyu.

<sup>74</sup> Naye akasema, “Ninajua Mtu huyo hakumjua. Basi nilienda nyumbani na kuchunguza jambo hilo katika Maandiko, ndipo nikakuta kwamba *hiyo* ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi. Ndipo basi wakati nilipokuwa nimesimama pale, nami ni—nilikuwa nimesimama upande wa pili, bila shaka, pamoja na makuhani, na ndugu zangu, na kusikiliza kuona kile ningeweza kusikia kikisemwa. Nao hao ndugu, wakasema, “Tutafanya nini tutakaporudi?”

<sup>75</sup> Wakati Filipo alipokuja na kumleta Nathanaeli, na kwamba Yesu alisimama pale na kumwambia Nathanaeli kwamba yeye alikuwa ni nani, na mahali alipompata, na kadhalika namna hiyo. Nasi tulimwona Nathanaeli, alikuwa, labda, akisomea kuwa mhubiri, basi akasema, “Mbona, Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu, Mfalme wa Israeli.”

Akasema, “Unaamini kwa sababu nilikwambia hivyo?”

<sup>76</sup> Na labda alikuwa ameketi huko nje pia kumsikia yule mwanamke kisimani, na—na kusimama langoni wakati ule ambapo kipofu Bartimayo alikuwa huko nje akilia, “Yesu, Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu!” Asingeweza kumgusa. Kama ukienda kwenye... Kama uliwahi kuwa mahali hapo, waliweka alama mahali Bartimayo alipokuwa ameketi na mahali Yesu alipokuwa wakati alipomwita, loo, jamani! Umati huo wote, ukipiga mayowe, ukisema, “Aisee, wananiambia ati unawafufua wafu, tuna makaburi yaliyojaa hao hapa juu, njoo huku, wafufue baadhi yao, tutakuamini.” Mnaona? Angewezaje kamwe kusikia yote...? Lakini imani yake ilimgusa.

<sup>77</sup> Kama vile maskini Zakayo, niliyewaambia Wafanyabiashara Wakristo, ameketi juu ya mti namna hiyo, kasema, “Sasa, Rebeka aliniambia ya kwamba Yeye—Yeye alijua mambo yote na angeweza... Mungu alinena kupitia Kwake Naye alikuwa ni Masihi, kwa hiyo nitavuta matawi haya yote karibu nami, na—na Yeye kamwe hatajua nimeketi hapa juu.”

<sup>78</sup> Kwa hiyo wakati Yesu aliposimama moja kwa moja chini ya mti na kuangalia juu, na kusema, “Zakayo, shuka chini; nitaenda nyumbani pamoja nawe,” kwa hiyo labda, alikuwa hapo asubuhi hiyo kuona jambo hilo. Hata hivyo, aliamini ya kwamba kupitia kwa Maandiko kwamba Huyu alikuwa ndiye Masihi.

<sup>79</sup> Na, lakini hata hivyo asingeweza kufanya maungamo kwa sababu shirika la wahudumu la Gadara lilikuwa limesema hivi: “Kama kuna mtu yeyote atakayehudhuria mmoja wa hiyo miamsho ambayo nabii huyo wa Galilaya, kule, anafanya, tutamfukuza wakati uo huo kutoka kanisani.” Vema sana, ye—yeye... walikuwa na mchungaji hata hivyo, na—naye alikuwa na kusanyiko kubwa, na kundi zuri la watu, na—naye alijua

alimpenda Bwana, lakini moja kwa moja moyoni mwake, alijua kulikuwa na kitu kingine kinachopaswa kuongezewa.

<sup>80</sup> Loo, Zakayo, natumaini umeketi hapa usiku wa leo, wala usiamke na kutoka nje mpaka hili litakapokwisha, unaona. Tulia tu kwa dakika moja.

<sup>81</sup> Naye huyo hapo, mwajua, huko nje, huku anaamini hilo, kisha akaja nyumbani kwa nuru ndogo ya mshumaa, na kusoma usiku kucha, wakati angeenda kwenye mmoja wa mikutano hiyo, na kusikiliza, labda alificha sura yake, na kuweka utaji juu ya uso wake, ama chochote kile, asije akajulikana kama Dk. Za- . . ., ama, Dk. Yairo, mwajua, ama, asingetaka tu kujulikana miongoni mwa umati. Lakini hata hivyo, alikuwa ameketi pale, naye aliangalia hili, na akalichunguza, lakini hata hivyo, asingeweza kumkiri waziwazi, hadharani, kwa sababu ingembidi kuachana na ushirika wake wa wahudumu na ushirika wake pamoja na ndugu zake. Na hiyo ndiyo sababu hao wote pamoja walimfukuza Yesu kutoka Gadara, na kumrudisha katika nchi Yake Mwenyewe. Katika nchi Yake Mwenyewe, limekuwa ni jambo lile lile. Basi mtu yeyote aliyejiunga na huyu *anayejiita* Nabii wa Galilaya, mbona, ilibidi atengwe.

<sup>82</sup> Lakini mnajua, Mungu anayo njia ya kuleta hiyo imani halisi ya kweli ndani yetu, Mungu ana njia za kipekee za kufanya hivyo. Na kwa hiyo, hebu tuseme usiku mmoja yule msichana mdogo alikuwa ameingia, naye alikuwa. . . Alikuwa na binti mmoja mdogo, mwenye umri wa kama miaka kumi na miwili, naye alikuwa anazeeka, naye huyo alikuwa ndiye mtoto wa pekee yeye na mke wake walikuwa naye. Usiku mmoja msichana huyo alikuja akitoka kuruka kamba, ama kitu fulani karibu na parokia, naye akaingia, akasema, “Baba, mimi ni mgonjwa *sana*.”

Kwa hiyo akakigusa maskini kichwa chake na kusema, “Naam, Mpenzi, wewe ni mgonjwa.”

Kwa hiyo akasema, “Mama, hebu nikwambie, mlaze kitandani, nasi tutashuka tukamlete daktari.” Hilo ndilo jambo pekee la busara kufanya.

<sup>83</sup> Kwa hiyo wakaenda na kumleta daktari mzuri kutoka kwenye ujirani, naye akaja na kumgusa. Naye akasema, “Naam, ana homa kali.” Kwa hiyo akamtibu kwa siku mbili au tatu, ndipo akaja kugundua, homa yake ilizidi kuwa mbaya. Na, loo, ikafikia mahali fulani, akawa na joto sana, hata alikuwa anapata, daktari akaingiwa na wasiwasi juu yake. Kwa hiyo akajaribu mimea yote na tiba zote alizojua kujaribu kumsaidia msichana huyu mdogo, bali ha—hakuweza kufanikiwa kwa hizo, asingeweza tu kuiondoa ile homa.

<sup>84</sup> Kwa hiyo basi asubuhi moja yapata saa tatu, mbona, alikuwa amekuja kumtembelea huyo msichana mdogo baada ya kuwa macho karibu usiku kucha. Ndipo watu wote wa kanisa

wenye upendo walikuwa wamekusanyika mle ndani, na—na wachungaji wenzake wote, na baadhi ya makasisi wageni, na mzee wa wilaya, na wote walikuwa wameketi karibu, mwajua, ku—ku—kufanya maombi, na kadhalika, kwa ajili ya mtoto huyo.

<sup>85</sup> Na kwa hiyo, daktari akaingia chumbani, naye akamchunguza maskini msichana huyo, akachukua mapigo yake ya moyo, na, loo, homa ilikuwa kali sana. Maskini huyo mtoto alikuwa amepita, ameingia wazimu sasa. Kwa hiyo alijua ya kwamba mwisho ulikuwa umekaribia. Alichukia kumwambia mchungaji; labda, alienda kwenye kanisa lake mwenyewe. Kwa hiyo akamwita kando, na kusema, “Sasa, Yairo, ninataka kukwambia hapa nje, ili *Dada* asije akasikia, mtoto huyo yuafa, maskini msichana wako wa pekee.”

“Loo, Daktari! Hakika kuna jambo lingine unaloweza kufanya.”

<sup>86</sup> “La, Yairo, kama—kama unataka kumwita daktari mwingine na kutafuta ushauri juu ya huo ugonjwa, mbona, hilo ni sawa. Lakini kwa ufahamu wangu wa matibabu, kifo kiko juu ya mtoto huyo sasa hivi, kwa sababu yuko katika hali ya kufa, na labda hatadumu zaidi ya saa nyingine moja au mbili.” Yule daktari mzuri alikuwa akisema yote aliyojua kuwa ni kweli.

Kisha kasema, “Daktari, ungenishauri nimtafute daktari mwingine?”

Kasema, “Umekaribishwa.”

<sup>87</sup> Lakini akasema, “Simjui daktari mwingine. Tunajua kulikuwa na daktari ng’ambo ya . . . kule, aliyeitwa Luka, Dk. Luka, lakini, unajua, a—aliongoka.”

“Loo, usininii . . . Luka amepotoka.” Mnaona? “Anamfuata yule nabii wa Galilaya, usininii . . .”

Loo, hilo linamkumbusha. “Naam, Daktari. Vema, asante. Unaidai nini, Daktari?”

<sup>88</sup> “Loo, vema, mimi . . . hiyo ni sawa, haikubidi kunilipa chochote.” Alikuwa ni mtu mzuri. Mnaona? “Wewe endelea, Mhubiri, najua hupati pesa nyingi, kwa hiyo acha tu.”

“Vema, asante sana.”

<sup>89</sup> Sasa, atafanya nini? Anarudi kutoka langoni na kusema, “Sasa, nitaingia nyumbani kule, parokia. Na nini . . . Nitamwambiaje mke wangu ya kwamba mtoto huyo yuko katika hali ya kufa? Nami nimemficha wakati wote kwamba kweli niliamini Yesu kuwa ndiye Nabii *halisi*, aliyekuwa aje. Lakini sasa, ningelipataje? Na kuna yule mzee wa wilaya na wengine wote wa shirika la wahudumu wameketi nyumbani pale. Basi ninawezaje kamwe? Wala sijui mahali alipo Yeye.”

<sup>90</sup> Kwa hiyo anarudi chumbani, naye anaanza kushangaa. Na, mnajua, na, muda si muda mwajua, anamwita mkewe ndani,

akasema, “Mpenzi, ingia na uketi chini kwa dakika moja tu.” Akaweka mikono yake, akasema, “Sasa, nina jambo fulani ninalotaka kukuzungumzia. Kwanza, nataka kusema, Mama, unakumbuka jinsi ambavyo nimeketi hapa usiku, miangaza hii ya mishumaa, nikisoma Maandiko?”

“Ndiyo, ndiyo, Yairo, na—na—najua jinsi ambavyo umeketi hapa na kusoma.”

“Nami nimeingia, nikiondoka kwa siku mbili ama tatu kwa wakati mmoja, nikikwambia nilikuwa nje kwa ajili ya kazi ya Bwana.”

“Ndiyo, ninakumbuka yote kulihusu.”

“Vema, nimekuficha hili, lakini nataka kukwambia jambo fulani. Unajua mahali nilipokuwa?”

“Vema, ulikuwa wapi, Mpenzi?”

“Nilikuwa nikihudhuria mikutano hiyo ya Yesu wa Nazareti, yule Nabii wa Galilaya. Nilikuwa nikihudhuria. . .”

<sup>91</sup> “Loo,” akasema, “hiyo si siri kwangu, nilikuwa nikisoma muhtasari wako ulioandika wa Mahubiri Yake, unaona. Nilipokisafisha hicho chumba, nilikuta kikapu cha taka kimejaa huo, unaona. Nami niliusoma tu ambapo mmekuwa mkichunguza Maandiko.”

“Kweli kabisa?”

“Ndiyo.”

“Vema, nakwambia, unajua nini? Kweli ninaamini ya kwamba Huyu ndiye Masihi.”

“Mbona,” akasema mke, “Mpenzi, hivi uko tayari tu sasa kukiri jambo hilo? Niliamini hilo wakati wote.”

Sasa, yeye yuko tayari, anaweza kumwambia sasa, kilicho. Kasema, “Unajua nini?” Kasema, “Mpenzi, daktari ndio kwanza aniambie jambo fulani.”

“Nini? Binti yetu atapata nafuu?”

“La, yuafa.”

“Loo, Yairo! Loo, loo, hakika, sivyo!”

<sup>92</sup> “Naam, naam, yu—yu—yuafa. Lakini nashangaa alipo Yesu wa Nazareti. Wajua, Yeye—Yeye aliondoka na kuvuka bahari siku chache zilizopita, Naye ameondoka, nami si—sijui aliko. Laiti tungaliweza tu kumpata! Vema, vema, afadhali tuungame imani yetu na tuondoke.

<sup>93</sup> “Vema, tuliondoka, siku moja kabla ya ninii, watu wote na kusema, ‘Vema, sina budi kutangaza jambo fulani: Daktari ndio kwanza aniambie kwamba mtoto wangu yuafa, msichana wangu wa pekee, mwenye umri wa miaka kumi na miwili, yuafa.’” Na kwa hiyo, anasema, na wote wanaanza kuomboleza, na kulia, na kuendelea.



<sup>94</sup> Akasema, “Sasa, ngojeni, hilo silo tumaini letu la mwisho. Hebu kidogo.” Loo, ninahisi maskini uso wake ukiwa mwekundu, alimtazama mzee wa wilaya, na askofu, na hao wote wameketi karibu, mwajua. Basi atafanya nini? “Lakini tuna Tumaini jingine.”

Nami ninaweza kumsikia askofu akisimama, akisema, “Vema, unataka kushauriana na daktari mwingine?”

“Vema, la, sivyo hasa. Lakini nina kitu fulani. . .” Ndipo moyo wake ukaanza kupiga haraka sana, mwajua. Unaweza kulisema? Akashikwa na kigugumizi kidogo.

Nami ninaweza kumsikia mke wake akisema, “Endelea, waambie, waambie, waambie!”

<sup>95</sup> “Vema, uh, *ahem*, uh, ndugu, *ahem*, naam, najua hili huenda likawasumbua kidogo tu, *ahem*, lakini, uh, naam, ninaamini ya kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu. Ni—ninaamini ya kwamba Yeye, yule Nabii wa Galilaya ndiye Masihi. Nimekuwa. . .”

<sup>96</sup> Mbona, ninaweza kumwona askofu akisimama, na mzee wa wilaya, na watu wote mashuhuri, na kusema, “Mbona, Yairo! Jamani, humaanishi umeenda kama Luka na hao wengine walivyofanya?”

“Naam, ninamwamini Yeye, hakika ninamwamini.”

<sup>97</sup> Kwa—kwa—kwa nini? Alikuwa na haja. Mungu anayo njia ya kuliweka juu yako hivi kwamba, atakufanya utoke ukiwa na imani hiyo, uitoe tu moja kwa moja kwa vyovyote vile. Naam, bwana.

Sasa, ningeweza kumsikia akisema, “Kuna mtu anayejua mahali Yeye alipo?”

<sup>98</sup> Jamaa mmoja mdogo akasema, “Naam, ni—nilikuwa mgonjwa hivi majuzi, nami ni—nikashuka kwenda kule kumwona Dk. Luka, na Luka yuko pamoja Naye, na Yeye—Yeye alikuwa huko Gadara, nao, nilisikia kwa tarishi kwamba wanakuja leo. Wanapaswa kufika asubuhi ya leo huko chini kwenye bandari ya kuvulia samaki.”

Ninaweza kumwona maskini Yairo akitoka nje na kuchukua kofia yake ndogo ya kuhani, na kuivaa, akivaa koti lake, akaondoka.

<sup>99</sup> Ninaweza kumsikia mzee wa wilaya akisimama mlangoni, akisema, “Sasa, angalia hapa, kijana mwanamume, sasa, umekuwa mmoja wetu kwa muda mrefu, sasa, kama utanzisha kitu kama hicho na kulichanganyisha kusanyiko letu, kuleta ulokole kama huo katika kundi letu, unajua kitakachotukia? Tutakufukuza, tutaondoa jina lako moja kwa moja kwenye kitabu, hivyo tu.”

<sup>100</sup> Vema, ninaweza kusikia maskini moyo wake ukizama, namna *hiyo*. Akageuka akamtazama mkewe, naye alikuwa amesimama akiona yale atakayosema, kisha akaangalia na kumwona binti yake mdogo, anayekufa, akasema, “Afadhali uliondoshe, maana mimi huyu hapa naenda.” Hiyo ni kweli. “Naenda zangu.” Alikuwa na haja. Akiharakisha, hana budi kwenda *sasa hivi*.

Wakasema, “Kumbuka, kama ukienda, unajua kitakachotukia, unajua tangazo letu.”

<sup>101</sup> “Naam, ninaelewa yote kulihusu. Lakini nina mtoto anayekufa hapa, na jambo lile lile ambalo nimeficha moyoni mwangu wakati wote, nimeyachunguza Maandiko, nimehudhuria mikutano Yake kwa kuficha utambulisho wangu, nami nimeyachunguza Maandiko, Naye *ndiye* Masihi!” Amina. Jambo ndilo hilo. Amina. Hiyo ndiyo njia ya . . . Sasa unaifikia, Yairo. Njoo moja kwa moja ukawaambie yaliyo sahihi. Kiri imani yako, ndipo unapata, haki yako, kwenye njia sahihi basi. Kwa—kwa—kwa namna fulani haionekani yenye majonzi.

Loo, akasema, kanisa likasema, “sasa, unakumbuka, kama ukifanya hivyo, vema, kitakachotukia.” Lakini Yairo alikuwa na haja.

<sup>102</sup> Haja! Basi ndugu, kama kuliwahi kuwa na wakati, ndugu, ambapo tunapaswa kukiri kwamba Yeye ni Masihi, Mwana wa Mungu, ya kwamba Yeye yu hai, kwamba—kwamba nguvu Zake ni zile zile, kuna haja leo, leo ndiyo wakati, watu wanakufa. Watu wanakufa makanisani. Watu ni . . .

<sup>103</sup> Kanisa la Kipentekoste linakufa, linaingia baridi sana. Linaenda mbali na Mungu. Kama kuna wakati wowote wa kutoka na kusema, “Tunakufa, hebu tumrudie Mungu,” ni sasa hivi, kwa sababu kuna haja. Rudini kwenye ile imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja.

<sup>104</sup> Ninajua kuna ulokole mwingi, ninatambua hilo. Na kama nilivyosema kwenye kiamshakinywa cha wahudumu hivi majuzi asubuhi, ni vigumu kuwalaumu wachungaji, lakini kumbukeni, kila wakati mnapoona kitu cha uongo, dola bandia, ni hakika tu kama kitu chochote ulimwenguni imefanyizwa kutokana na iliyo halisi.

<sup>105</sup> Kamwe sikushangaa sana, wakati mmoja, nilikuwa nikipanda barabarani, nami nikaona ku—ku—kundi kubwa la kunguru, ama ndege weusi, walikuwa tu na wakati mbaya sana wa kilio kirefu cha hofu. Nikawaza, “Kwani wana shida gani?” Nikaendelea kupanda barabarani, na kulikuwa na baadhi yao waliokuwa mitini, na wengine kwenye nguzo za simu, huku wengine wameketi kwenye nyua, nikawaza, “Hivi hawa ndege wana shida gani?”

<sup>106</sup> Kulikuwa na shamba la stroberi upande wa pili wa—wa shamba, naye mwenye hilo shamba alikuwa ameenda likizoni

Florida, naye akaziacha tu hizo stroberi pale, asingeruhusu mtu yeyote kuzichuma, kwa sababu a—alipenda kuona . . . aliziweka pale kwa ajili ya ndege, alipenda tu kuwaangalia ndege. Na kwa hiyo, wakati alipokuwa ameshuka kwenda Florida likizoni, mbona, mtu fulani alikuja pale na kuweka maskini sanamu ya kutishia shambani, nao walitaka kuchuma hizo stroberi wenyewe, sio kuwaachilia hao ndege wazile.

<sup>107</sup> Hao ndege walikuwa wamesisimkwa sana. Loo, jamani, walisisimkwa sana! Baadhi yao wameketi *mbali* sana kwenye mti, wakiziangalia hizo sanamu za kutishia kule, na—na ku—kulia tu na kulia tu, na kuendelea, wengine wameketi kwenye nguzo za simu, na wengine wameketi kwenye nguzo za ua, nami nikawazia, “Vema sasa, sijui kuna nini?” Basi ilitokea niliangalia, ndege wawili, wenye afya, wameketi papo hapo mikononi mwa hizo, maskini sanamu hiyo ya kutishia, wakila tu kwa nguvu walivyoweza kula. Nikawaza, “Kama hiyo si picha hasa! Kama hilo si jambo fulani!”

<sup>108</sup> Sasa, nikawaza, “Vema, kuna nini?” Nikasogea karibu kidogo, nikaangalia, kuna stroberi nyingi sana, nikawaza, “Kuna nini, jamani?” Na hivyo ndivyo baadhi yao wafanyavyo. Baadhi yao, wataenda mbali, waende *huku* nyuma kabisa, hawaamini katika Roho Mtakatifu wala chochote kile. Wengine watapanda juu na kusema, “Vema, ninaamini katika maisha mazuri, yaliyotakaswa, lakini kamwe si—si—si—siamini katika uponyaji wa Kiungu.” Lakini wengine watashuka moja kwa moja karibu na mpaka, bali wanaogopa sanamu ya kutishia. Na hapo karibu ndipo Pentekoste imefikia sasa, mnaogopa sanamu ya kutishia.

<sup>109</sup> Mbona, ndugu, sanamu ya kutishia ni tiketi ya posho. Amina. Ingia tu nyuma ya sanamu hiyo ya kutishia, hilo tu ndilo unalopaswa kufanya. Ukiona kila namna ya itikadi za uongo na kadhalika zikiinuka, yale niliyosema hivi majuzi usiku, *itikadi* hizi zote karibuni zitakuwa *itikadikale*, kwa hiyo wao—wao ni—wao ni, usihofu juu yao, bali Neno la Mungu litakuwa kweli. Wakati hakuna tena Mbingu na nchi zilizosalia, bado litakuwa ni kweli. Naam, bwana.

<sup>110</sup> Hakukuwako na hukumu kwao, wameketi pale, wakila stroberi, ndugu, walikuwa wameketi pale, ndege wakubwa, wenye afya, wakidona tu kwa nguvu walivyoweza, kwa sababu hawakuwa wakijali ile sanamu ya kutishia, wa—wa—wao walikuwa tu wakila stroberi vivyo hivyo. Kwa hiyo hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya. Unapona mambo haya unayopata, kila mtu anazungumza vizuri sana, nalo kanisa linakuwa la hali ya juu, na yule jamaa *mkubwa* akisema, “Vema—vema, tutawaingiza tu kupitia *hili* na *lile*,” afadhali uwe mwangalifu, ndugu, kuna kasoro fulani hapo, mahali fulani, kuna kasoro fulani. Ninapenda kufikia ambapo mtu fulani anakosolewa na kudhihakiwa, kisha niangalie pande zote nione ni wapi . . .

nini. . . niyachunguze tena na kuona yote yanahusu nini. Naam, bwana. Ni kengele ya chakula cha kutwa, angalia tu moja kwa moja nyuma yake.

<sup>111</sup> Mnakumbuka, rungu daima hukaa chini ya mtofaa mzuri. Hawatengenezi rungu kutoka kwa maskini vifundo hivyo, vilivyokunjamana, vikali, “Siku za miujiza zimepita,” hakuna kitu cha kutengeneza rungu katika hilo, acha tu waendeleo.

<sup>112</sup> Lakini Yairo alikuwa na haja, naye alikuwa na haja kwa sababu mtoto wake wa pekee alikuwa yuafa. Na hilo ni jambo lile lile usiku wa leo. Sasa, haikumbidi kusema, “Sasa, nitangojea sasa. Huenda mimi, labda, kama ningengojea kidogo, huenda nikaenda kumwona kama Nikodemo alivyofanya, niende usiku. Nitaingia kisiri wakati mmoja usiku. Nakwambia. . .” Kamwambia, huenda alimwambia mke wake kitu kama hiki: “Vema, sasa huyo *hapo* mzee wa wilaya ameketi huko nje, na huyo *hapo* ameketi askofu, hilo hapo kanisa zima limeketi na kadhalika, nakwambia, nitangojea mpaka ifike usiku, ndipo usiku ukifika, nitavaa maskini kinyago changu tena, nami nitaingia kisiri mkutanoni. Na baada ya kumalizika, sitaacha mtu yeyote ajue, nitaingia nyuma ya jengo kisiri, niseme, ‘Aisee, Nabii wa Galilaya, ninakuamini Wewe, ninakuamini Wewe. Njoo huku, nina binti mgonjwa.’” La, binti huyo alikuwa yuafa *papo hapo*, ilibidi aende wakati *huo*. Ulikuwa ni wakati wa matendo.

<sup>113</sup> Basi ni wakati wa matendo, ndugu. Si wakati wa kubishana kuhusu kama tunapaswa kubatizwa kifudufudi, ama kinyumenyume, ama kama tunapaswa kuwa wafuasi wa kanisa *hili*, ama kanisa *lile*, ni wakati wa Roho Mtakatifu kuingia Kanisani na kuingia katika matendo. Muda umeenda sana kuliko mnavyodhania. Saa imewadia, sio wakati wa kuzozana juu ya kanuni za imani na juu ya mafundisho na mambo kama hayo, ni wakati wa kuingia katika Roho wa Mungu na kusonga mbele, maana mabomu ya atomiki yananing’inia, na makombora kila mahali, na sputniki angani. Na kila kitu ambacho Yesu alisema kingetukia kabla ya wakati wa mwisho kinatukia sasa. Naye Roho Mtakatifu yuko hapa, Kristo, moja kwa moja kwenye wakati unaofaa, kwenye ratiba. Naam.

<sup>114</sup> Wakosoaji wanainuka. Nitasema jambo hili kwa sababu lilikuwa, niliomba liepukwe wakati mmoja, ndipo walipofanya hivyo, huyo ndugu akafadhaika sana kulihusu. Mimi. . . Sasa, nitalisema, maana liko kwenye kanda, na kwa hiyo ndugu yetu anaweza kulisikia kama anataka kuchukua kanda hii. Ni kuhusu Ndugu David duPlessis, ndugu yangu wa thamani, rafiki.

<sup>115</sup> Nilipata barua ya ukosoaji kutoka kwake, na—nami sikutaka kuisoma, katibu aliipata, na kwa hiyo, si—sikutaka kuisoma. Ilikuwa ni kwa sababu nilijizuia sikutaja jina lake kwenye kanda. Lakini hii inarekodiwa, kanda zinaenda. Hivi ndivyo nilivyosema hasa: Nilikuwa nikihubiri juu ya kukaribia

kwa kuja kwa Kristo. Basi Ndugu David anashughulika na Wapresbiteri, Wamethodisti, na Wabaptisti, na hao watu mashuhuri. Hiyo ndiyo huduma yake kwao. Mungu amemtuma na huduma. David ni mwanatheolojia hodari, msomi, na mtu mzuri sana wa Mungu. Amekuwa pamoja nami mikutanoni, amesimama kando yangu. Ninampenda kama vile tu ndugu angeweza kumpenda mwingine, na hiyo ni kweli.

<sup>116</sup> Lakini yale niliyosema juu ya David, na kanisa litanishuhudia, nilisema, “Inaonekana kana kwamba Ndugu David, jinsi alivyo wa kiroho, angeamkia ukweli kujua ya kwamba anashughulika na bikira aliyelala. Nao Wapentekoste wanafurahi sana kuona Wapresbiteri wakiandika katika azimio dogo, ‘Vema, hatuna budi kurudi kwenye waponyaji wa Kiungu. Hatuna budi kurudi kwenye kunena kwa lugha.’”

<sup>117</sup> Mmesoma yale makala ambayo waliandika, “Hatuna budi kurudi kwenye ibada za uponyaji.” Billy Graham akizungumza, “Hatuna budi kurudi kwenye Pentekoste.” Hivi unatambua, ndugu, ya kwamba saa ile ile waliyoenda kumwamsha yule bikira aliyelala, wakati alipokuja kununua Mafuta, hapo ndipo Yesu alipokuja?

Nikasema, “Sijui kama Ndugu David anatambua hilo.”

<sup>118</sup> Mnafikiri kanisa la Kipentekoste, walikuwa na picha yao gazetini hivi majuzi wakiwa na baadhi ya makasisi wa Katoliki, wamesimama, wakibariki kiamshakinywa cha mfanyabiashara wa Kipentekoste, ama kitu kama hicho, na mambo kama hayo, ambayo hayo ni sawa, lakini nashangaa kama kanisa kweli linatambua ni kitu gani. Ni ishara. Wakati bikira huyo aliyelala alipokuja na kubisha langoni, hapo ndipo asingeweza kuingia, kwa kuwa Bibi-arusi alikuwa ameondoka, hivi hamwoni?

<sup>119</sup> Hivyo ndivyo nilivyosema kuhusu Ndugu David. Mnaona, si chochote kuhusu kazi yake, wala ninii yake. . . ama, kuhusu sifa zake. Naye David ni ndugu yangu, na mmoja wa watu walio bora sana, watauwa niwajuao, lakini nilishangaa tu jinsi ambavyo yeye—yeye hakuelewa hilo, kutambua dakika ile ile ambayo ulimwengu huo wa nje wa kimadhehebu unapoanza kuupokea Ujumbe huu, hiyo ndiyo saa hasa Yeye atakapokuja. Wakati wao—wakati walipoenda, yule bikira aliyelala alitambua hakuwa na Mafuta yoyote katika taa yake, ndipo wakati alipokuja kubisha mlangoni ayapate, huo ndio wakati hasa Bibi-arusi alipotoka, wakati yule bikira mwenye busara alipoondoka. Hiyo ni kweli. Hawakuingia, la.

<sup>120</sup> Nayo hayo madhehebu hayataingia. Hawatakuwa na nafasi ya kuingia, wakati Ujumbe utakaponezwa, Kanisa litakuwa limeondoka. Kwa hiyo kama wanajaribu kuingia sasa hivi, tuko karibu kiasi gani? Tunapoona kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu. Ujumbe ule wa mwisho kabisa, Ibrahimu na Uzao wake

baada yake, tunaona kila, kila kitu kiko kwenye wakati wake hasa. Tuna haja, ni wakati wa matendo. Sio, “Ngojeni mpaka niende shuleni nipate Ph.D., ama LL.D,” ni, “Ingieni katika Injili sasa hivi, hubirini.” Naam. Nendeni huko nje sasa, sasa ndiyo wakati.

<sup>121</sup> Yairo asingeweza kungojea mpaka kesho, mtoto wake alikuwa yuafa. Ndugu, hatuwezi kungojea madhehebu mapya, hatuwezi kungojea kitu fulani kichoche, tayari iko hapa. Hatuna budi kumleta Kristo jukwaani. Kanisa la Kipentekoste linakufa. Amina. Waassemblies, wa Umoja, wa Uwili, wa Utatu, wa—wa Foursquare, wote hao, wanakufa, hebu tuyaache mambo haya. Yote ni sawa, lakini msinini. . . acheni tu kuzozana juu ya jambo hilo, hebu na tumlete Kristo jukwaani.

<sup>122</sup> Hivyo ndivyo Yairo, ilivyombidi kumleta Kristo jukwaani la sivyo mtoto wake angekufa. Hana budi kuharakisha upesi sana, hana budi kuingia kazini upesi sana. Loo, ninapenda hilo. Ingia kazini.

<sup>123</sup> Loo, kama kundi hili, papa hapa usiku wa leo, ninyi Wamethodisti, ninyi Wabaptisti, ninyi Wapresbiteri, ninyi Wapentekoste, Umoja, Uwili, Utatu, na ninyi nyote, kama mungeingia kazini, mkiweka kando mapokeo yenu na uovu, mumlete Kristo jukwaani; ufungue moyo wako, Yeye yupo hapa. Amina. Mashua yake ndiyo kwanza iwasili, haleluya, jukwaani.

Mtu fulani alisema, “Naam, imani chanzo chake ni kusikia.”

Kasema, “Naam, Yeye anaingia kutoka bandarini kule chini sasa. Chini tu ya kilima kutoka kwenye parokia, anashuka kule chini sasa.”

Vema, huyu hapa anaenda, ananyakua maskini kofia yake, na, “Sijali wanayosema.”

<sup>124</sup> Wakasema, “Vema, Yairo, utasikitika moja ya siku hizi. Unajua, unarukia wendawazimu.” Hakujali wazimu wala *nini*, alijua kile moyo wake ulichomwambia.

<sup>125</sup> Wala hakuna mtu hapa ndani usiku wa leo, ila kama ungefanya yale moyo wako uliyokwambia ufanye, labda ungekuwa kwenye madhabahu hii. Kweli!

<sup>126</sup> Hakuna mhubiri aliyepo, kama ungefanya yale moyo wako uliyokwambia ufanye, ila ambayo tungeweza kuungama makosa yetu. Hiyo ni kweli. Unapokiri: “Jamani, niko tayari kuunganisha mikono na mioyo pamoja na watu kumleta Kristo jukwaani.” Hilo ndilo jambo muhimu. Watoto wanakufa.

<sup>127</sup> Kitabu hiki kidogo *hapa* kina hilo ono ndani yake. Nilipoangalia kule, hawakuninii. . . sikuninii. . . Nilipoenda hadi langoni, hawakuniuliza kama nilikuwa Mpentekoste wa Umoja, ama wa Utatu, ama wa Utano. Jambo pekee lililokuwa, Yeye aliniruhusu tu niingie, kwa sababu nilikuwa nimempenda

Kristo, na nilikuwa na upendo moyoni mwangu. Jambo ndilo hilo sasa, ndugu.

<sup>128</sup> Ilimbidi Yairo kuharakisha, mtoto wake alikuwa yuafa. Mtoto wa Mungu anakufa, kanisa linakufa. Hatuna budi kufanya jambo fulani. Huenda uliliita telepathia, huenda uliliita ibilisi, huenda. . . Sijui uliliitaje, lakini kama ndani kabisa ya moyo wako, kama uliamini ilikuwa ni kweli, ndugu, afadhali uweke kofia yako ya kikanisa pembeni, na useme jambo fulani, na uendelee kusonga mbele. Vema. Kanisa linakufa. Tunamhitaji Kristo jukwaani. Wakati wa matendo. Sio “Ninapojisikia hivyo,” sio, “Ninapochukua wazo lingine.” Lakini ilimbidi kuwaleta watu jukwaani, kwa sababu ninii, ama, kumleta Yesu jukwaani, kila kitu kingine kilikuwa kimeshindwa.

<sup>129</sup> Ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Je, kanisa la Kipentekoste liko afadhali zaidi usiku wa leo kwa sababu lilijigawa katika madhehebu thelathini mbalimbali, au wakati lilipoanza hapo mwanzo? Mnaona? Uliza tu hilo. Tunazidi kuwa wabaya zaidi na zaidi. Je, wanawake na wanaume katika makanisa yetu ya Kipentekoste wanaonekana zaidi kama watakatifu, wakiomba? Niambie mahali fulani mjini ambapo wanafanya mkutano wa maombi usiku kucha, siku baada ya siku, kwa ajili ya dhambi zinazotendwa mjini, kama walivyokuwa wakifanya. Je, sisi ni bora zaidi? Tunakuwa wabaya zaidi.

<sup>130</sup> “Loo, majengo yetu yanakuwa mazuri zaidi.” “Loo, tunakuwa bora zaidi katika ushirikiano na makanisa mengine.” Lakini ni nani anayetaka kuwa kama *wao*? Ninataka kuwa kama Yesu. Na hapo ndipo kila mtu anapaswa kutaka kuwa, kama Kristo, hebu na tumlete jukwaani. Mnaona? Nasi ni. . . Ma—ma—makanisa yanakufa, kwa hiyo hatuna budi kufanya jambo fulani, hatuna budi kuharakisha. Hatuna ninii yote. . . Hatupaswi kungojea mpaka—mpaka kwenye ule Utawala wa Miaka Elfu kufanya hivyo. Kama tutafanya hivyo, hatuna budi kufanya sasa, la sivyo litakufa. Jambo fulani litatukia.

<sup>131</sup> Huyu hapa anasema, “Sijali.” Maskini uso wake ulikuwa mwekundu. Ndugu, kila wakati alipopiga hatua, aliwazia, “Ninaendelea kuwa bora zaidi na zaidi wakati wote.” Anza tu wakati mmoja, uone kitakachotukia. Muda si muda mwajua, ilitokea kwamba aliangalia chini ubavuni mwa kilima, na ni jambo gani lililokuwa likitukia? Maskini mwanamke mmoja aliyemjua, labda wa parokia yake mwenyewe, alikuwa ameketi juu ya kilima. Naye alikuwa amejua kwamba alikuwa amezungumza naye kuhusu jambo hilo. Naye alikuwa amesema, waziwazi kabisa, alisema wakati mmoja, labda ilikuwa ni kitu kama hiki: “Yairo, unajua nini? Ninaamini ya kwamba yule Nabii kule ni Mtu wa Mungu.”

<sup>132</sup> “Vema, sasa, Dada, nisingeninii. . . Una—unaonaje kuhusu

hilo?” Bila shaka, ilimbidi kuwa mwangalifu ajue kama alikuwa tu ni mtego kutoka kwa baadhi ya watu wa wilaya au la, mwajua.

Kwa hiyo kasema, “Vema,” kasema, “umewahi kumsikia?”

“Loo, naam, mara moja moja nimemsikia.”

<sup>133</sup> “Mbona, sijawahi kumsikia, bali nimesikia habari Zake.” Kwa hiyo imani chanzo chake ni kusikia. “Na hebu nikwambie, ninaamini kama—kama ungeweza kumpata mtu wa kunivusha baharini kule, kwenye mashua mahali fulani, ama, mahali Yeye alipo, kama tu ningeweza kumgusa Yeye, ningeponywa.”

Naye huyu hapa anakuja, maskini uso mdogo, mwembamba sana, uliopauka, akishuka ukingoni. Mwangalie akiyumbayumba, akishikilia kitu fulani.

Na huko, wote wako kule chini, wakisema, “Habari za asubuhi, Kasisi.”

“U hali gani, Daktari? Tuna furaha kuwa nawe hapa.”

Na, “Rabi, nina furaha kuwa pamoja nawe tena. *Ahem, ahem,*” wanaangaliana, mwajua.

<sup>134</sup> Maskini Yairo akisimama pale juu, mwajua, kwa namna fulani kutupa tu ninii—ninii. . . Mwajua, kulikuwa na watu wengi sana waliomwamini, kwa hiyo ilimbidi kuwa mwangalifu, mwajua, yale waliyosema. Kwa hiyo akarudi, baada ya kitambo kidogo maskini mwanamke huyu, yeye. . . Akasema, “Waweza kunisaidia, bwana mwema, kufika kule kuninii. . . Ningependa kuzungumza Naye?”

<sup>135</sup> “Loo, usiyasikilize hayo. Tumesimama tu hapa nje, tunaenda, tunajiandaa kumnasa. Tumemwekea mtego asubuhi ya leo, kweli tutamshika asubuhi ya leo. Wewe angalia tu,” mnaona, “sisi, hiyo ndiyo sababu, tunamwita, ‘Halo, hapo, Daktari. Halo, Rabi.’ Unaona, tumemwekea mtego, tutamfadhisha asubuhi ya leo.” Kwa hiyo hii. . . “Kwa sababu wanasema anajua siri za moyo. Tumeandaa yote kwa ajili yake.”

<sup>136</sup> Kama vile mtu fulani alivyonifanyia hivi majuzi usiku, naye akashindwa, wakati Roho Mtakatifu aliposhuka. Wala sijui kama mliona jambo hilo au la, lakini hakika lilitokea, lilikuwa ni kikwazo kikubwa kwa maskini mvulana huyu.

<sup>137</sup> Ndipo basi wakati—wakati wao, muda si muda mwajua, wakaja, kasema. . . Akashuka akaenda. Asingeweza kumfikia, kwa hiyo akashuka mikononi na magotini mwake, akaanza kutambaa katikati ya miguu yao, namna *hii*, mpaka akasimama. Na labda, maskini Yairo amesimama pale akimwangelia, wakati akiugusa ule upindo. Mtazamo mdogo, wa furaha, hata hivyo, ukaja usoni mwake, akarudi huko nje.

<sup>138</sup> Naye Yairo alikuwa amesimama akiangalia hilo, mwajua, akiangalia, kasema, “Nilimwona, nami ninamjua, ndipo akasogea pale na kuligusa vazi Lake, na sasa, amerudi huko nje,



naye anaonekana kana kwamba amefurahi. Anaonekana kama yule ambaye. . . Aliniambia wakati mmoja, kama angeweza tu kumgusa Yeye, hilo ndilo lingetukia, angepona. Nami najua madaktari walimkatia tamaa muda mrefu uliopita, tangu alipoanza kukata hedhi, akiwa na kutokwa huko kwa damu, amekuwa nako huko kwa miaka na miaka. Na kwa hiyo, maskini huyo, nilimhurumia. Mumewe aliuza farasi na kila kitu na kulipa bili ya daktari, wala hakupata nafuu zaidi ya alivyowahi kuwa. Yeye, maskini huyo, ninamhurumia.”

Yesu akasimama, akaangalia pande zote, akasema, “Uh, *ahem*, ni nani aliyenigusa?”

Naye akasema, “Mbona,” mtume akasema, “mbona, kila mtu anakugusa. Kwa nini—kwa nini unasema jambo kama hilo, Rabi,” ama—ama, “Bwana?” Yeye. . .

<sup>139</sup> Akasema, “Lakini ni—nilidhoofika, ni—nilihisi kitu fulani kikitoka ndani Yangu, nguvu zilinitoka.” Ndipo akamgeukia maskini huyo mwanamke, na kumwambia, kutokwa kwake na damu kulikuwa kumekoma.

<sup>140</sup> Ninawazia hilo lilimtia moyo mzee Yairo, je, wewe huwazii vivyo hivyo? Moja kwa moja huyu hapa anakuja, akikimbia mbio na kusema, “Bwana, msichana wangu mdogo sasa amelala mahututi.”

“Bwana,” akasema, “Mwalimu.” Loo, naam, yeye yuko sawa, yeye si shupavu wa dini sasa. Loo, la, huh-uh. Ana haja Naye.

<sup>141</sup> Huenda ukaiita hii kila kitu unachotaka, lakini moja ya siku hizi utakaposhuka moja kwa moja kitandani, itakuwa ni tofauti. Hiyo ni kweli. Hatakuwa ni mtakatifu anayejibingirisha, kundi la wendawazimu wakati huo, hiyo ni kweli.

<sup>142</sup> “Loo, Rabi, Mwalimu, Bwana wangu, msichana wangu mdogo amelala karibu kufa, kama utakuja tu na kuweka mikono Yako juu yake, a—atapona, yeye. . . kila kitu kitakuwa sawa. Daktari ndio kwanza aondoke tu yapata saa moja iliyopita. Rabi, ni—ni—ni—nimeacha kila kitu. Mi—mimi. . . Watanifuza kwenye shirika, kila kitu, lakini sikuzote ni—ni—nimekuamini. Lakini nakwambia, jambo fulani limetenda kazi, hata ikanibidi tu kulikiri, kwa hiyo mimi huyu hapa. Msichana wangu atakufa, na kama utakuja tu na kuweka mikono juu yake, hatakuwa, ataishi.”

Yesu akasema, “Nitaenda. Naam, nitaambatana nawe.”

<sup>143</sup> Naye akaendelea nalo hivyo. Nami ninaweza kuwazia kuhani akisema, “Ulisikia nini, na huyo ni nani? Vema, huyo ni Dk. Yairo. Jamani! Ungeweza kumwazia? Vipi kuhusu. . . ? Hivi hilo shirika halitamfukuza! Loo, amelipata sasa. Ndugu, kwenye kongamano lijalo hakika watammiminia hayo. Hebu na twende kule sote, Ndugu, tuone tu yale kuhani mkuu atakayosema, kile watakachonini. . . jinsi watakavyomtenga.”

144 Maskini Yairo hakujali, binti yake alikuwa yuafa. Naye alikuwa na ninii, aliuvutia usikivu wa Yesu, hilo tu ndilo alilojali. Na maadamu unapata usikivu Wake, kuna tofauti gani, chochote kingine kinaleta tofauti yoyote? Akitembea namna hiyo, na, anapoenda, akitembea, mwajua. Naye maskini mwanamke huyo alifurahi sana kwa sababu kutokwa kwake na damu kulikuwa kumekoma.

145 Ndipo basi muda si muda mwajua, huyu hapa mtu anakuja, juu ya kilima, akipiga makelele, “Usijisumbue, usijali.” Ndipo pigo la usiku wa manane likaja, loo, jamani, pigo hilo, “Aisee, Yairo, nilikwambia, haikukupasa kwenda kule chini. Unaona? Huyu hapa mzee wa jimbo anakuja na hao wote. Msichana wako alikufa yapata saa moja iliyopita. Nilikwambia. Siku za miujiza zimepita.”

146 Loo, jamani, pigo hilo la usiku wa manane, mwajua, maskini moyo wake ukaanza kurukaruka, akawaza, “Loo, loo, loo! Ni—nilimwambia kama angekuja aweke mkono wangu, uh, mikono Yake . . .”

147 Sasa, alikuwa na imani katika *mikono* ya Yesu. Hiyo ni . . . Yeye alikuwa ni Myahudi. Sasa, ilikuwa ni tofauti, Petro, usiku huo wakati alipokuwa akitembea juu ya maji, alipomwona Yesu akitembea, alidhani ilikuwa ni kivuli, akasema, “Bwana, ikiwa ni Wewe, niamuru nje.” Neno lilikuwa, “Njoo.” Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli.

148 Halafu ile siku alipokuwa akivua samaki, alivuta usiku kucha, hakuwa amekamata samaki hata kidogo. Alisema, akamwambia, kasema, “Naweza kuazima mtumbwi wako kwa dakika moja kuhubiria, Simoni?”

“Naam.”

Vema, Yeye alihubiri kutoka kwake kidogo. Kasema, “Sasa tweka mpaka kilindini mkashushe ili mshike samaki.” Mnaona?

149 Naye akasema, “Bwana, kama utaweka mikono Yako juu ya maji, ni—ni—ninaamini unaweza kuweka samaki mle. Tumefanya kazi ya kuchosha usiku kucha, tusipate kitu,” la, la, “Bwana, tumefanya kazi ya kuchosha usiku kucha, tusipate kitu, hata hivyo, kwa Neno Lako, nitashusha wavu.” Jambo ndilo hilo. “Kwa Neno Lako, nitashusha wavu.” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

150 “Nenda kwenye birika la Siloamu u—ukanawe.” Sasa, imani yake ilipaswa kuwasiliana na nini? Mara tu alipoweza kupata hilo birika. Mnaona? Kama angeweza kamwe . . . “Vema, ni njia gani ya kwenda kwenye birika la Aliyetumwa. Ni njia gani? Mtu fulani anisaidie kufika kwenye hilo birika.”

“Loo, unataka nini kwenye birika?”

“Haileti tofauti yoyote, nisaidie kufika kwenye birika, maana ninajua nitakapofika kwenye birika!”

“Mtu fulani anisaidie kwenda mkutanoni.”

“Vema, unaenda wapi?” Mnajua ninalomaanisha. “Usingeweka . . . ? Usingeenda kwenye kundi hilo sivyo?”

<sup>151</sup> “Vema, nisaidie tu niende kule, hilo tu ndilo ninalotaka kujua. Nipeleke kule.” Amina. Napenda hilo. Naam, bwana. Nipeleke kwenye kundi la watu ambapo ninaweza kuiona Biblia ikiishi, ambapo ninaweza kumwona Kristo akiishi ndani ya watu. Nipeleke miongoni mwa kundi hilo.

“Nisaidie kufika kwenye birika la Aliyetumwa.”

<sup>152</sup> Na punde tu waliposema, “Vema, haya basi,” mama fulani mwema, ama *yeyote yule* akaja, akamshika mkononi mwa—mwa—mwake, na kumpeleka kwenye birika, kasema, “Jamaa mzee, hili hapa lile birika, ni kwa nini?”

<sup>153</sup> “Loo, nimepata tu Neno la Mungu hivi punde lililoniambia nitakaponawa, nitaona.” Na, loo, jamani! Loo, akafunguliwa macho yake, ndipo akarudi akishangilia. Ilikuwa ni birika kwa ajili yake.

<sup>154</sup> Lakini wakati Mariamu, asubuhi hiyo ilipombidi kuchukua ninii . . . kushuka kwenda kuchota maji kisimani, naye akaangalia amesimama pale, na hapo palisimama Nuru kubwa, angavu, aliangalia Nuru hiyo, ilikuwa imemfunika Malaika aliyesema alikuwa ni Gabrieli, kasema, “Roho Mtakatifu atakutia uvuli, nawe utamzaa Mtoto, pasipo kumjua mwanamume yeyote,” akasema, “Tazama, mimi ni mjakazi wa Bwana, na iwe kwangu sawasawa na Neno lako,” Hilo tu ndilo alilotaka.

<sup>155</sup> Hakutaka kuninii . . . Hakusema, “Ngoja, sasa, nitakapotywa uvuli, halafu kama nikihisi uhai, basi nitaenda nikishuhudia? Nikiwa na yapata miezi minne, itakuwa sawa basi? Au ninapaswa kulishuhudia lini?” Hakuuliza swali lolote, alikuwa na Neno Lake, na hilo lilikuwa zuri vya kutosha kwake, akaanza kushuhudia papo hapo.

<sup>156</sup> Nami ninawapa Neno Lake: “Kwa mapigo Yake mliponywa.” Amina.

<sup>157</sup> Ninyi msio na Roho Mtakatifu, ninawapa Neno Lake: Petro alisema kwenye Siku ya Pentekoste, wakati wakosoaji walipokuwa wamesimama karibu, alisema, “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu.”

“Vema, a—askofu aliniambia, mzee wa kanisa aliniambia, mtu wa wilaya aliniambia, mchungaji aliniambia siku hizo zilikuwa zimepita.”

<sup>158</sup> Sijali walichosema, Biblia ilisema, “Ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa hao walioitwa, na kwa wote watakoitwa na Bwana Mungu wetu wamjje.” Hilo ni

Neno Lake, lipokeeni. Yeye alilituma Neno Lake. Hilo ndilo linalohitajika, Neno Lake. Lakini Yairo alitaka mikono Yake. Mwajua, nafikiri Mungu ni Mungu mwema, Yeye—Yeye aliweza kwa . . . kuingia mle kwa njia fulani.

<sup>159</sup> Mwajua, wengi wa wanafunzi, waliamini mara waliposikia neno ya kwamba Yesu amefufuka katika wafu, kasema, “Mungu asifiwe, hilo ni sawa.” Lakini Tomaso akasema, “Sina budi kuweka vidole vyangu kwenye alama za misumari mkononi Mwake. Sina budi—sina budi kuihisi, si—sina budi kuliona mwenyewe, nililiona likifanya kazi kwa wengine mikutanoni, bali halina budi kuwa juu yangu.” Loo, Thomas ana watoto wengi sana, lakini yeye . . . Lakini Mungu ni Mungu mwema, Yeye—Yeye hufanya kazi kote kwa vyovyote vile.

Akasema, “Njoo hapa, Tomaso, uniguse. Sasa, inatenda kazi juu yako. Unaamini, Tomaso?”

Kasema, “Loo, naam, Wewe ni Bwana wangu sasa. Ninaamini sasa.”

Akasema, “Ni kubwa zaidi jinsi gani thawabu yao ambao hawajaona na hata hivyo wanaamini!” Amina. Wanaamini Neno la Mungu kwake, hivyo tu. Amina.

Loo! Nami ndio kwanza tu ninafikia somo langu. Lilikuwa wapi? Hebu tuone. Loo, naam. Naam, bwana.

Basi ve—vema, hebu na tumchukue. Huyu hapa anarudi juu na hawa hapa wakosoaji wote wakitoka, mwajua, wakisema, “Huyo hapo anaenda zake.”

<sup>160</sup> Basi jambo la kwanza wakati yule tarishi alipokuja na kusema, “Vema, usijisumbue tena.” Kasema, “Yeye—yeye . . . Yule mtoto mchanga alikufa, amekufa. Tayari tumemweka huko juu, na amewekelewa maua, na ana nguo za kuhifadhi maiti, amemwagiliwa ugiligili. Wala hakuna haja ya kujipumbaza tena, huyo mtoto tayari amekufa. Daktari alirudi, tukaenda, tukamleta, naye akamtangaza amekufa, naye tayari amemlaza huko nje, na ni baridi, amewekwa chumbani kwenye kitanda cha mauti. Na—na waombolezaji wote wako huko, na kuna maombolezo kote huko, hujapata kusikia kitu kama hicho. Kwa hiyo . . .”

<sup>161</sup> Yesu, akitembea imara. Loo, ninapenda hilo! Hivi usingeweza tu kumwona, ndugu? Haikumsumbua hata kidogo. Maskini Yairo, moyo wake ulikuwa ukidunda, mwajua, akasema, “*Puu, puu,*” akaangalia huko.

Yesu, ninaweza tu kumwona akigeuza hayo macho na kusema, “Je, sikukwambia, ‘Amini tu?’” Loo!

<sup>162</sup> Hivyo ndivyo ninavyowaambia: Aminini tu Neno la Mungu kama mnataka kuona utukufu wa Mungu. Amini tu, haidhuru mtu mwingine yeyote anasema nini, jinsi ulivyo mgonjwa.

“Lakini, Ndugu Branham, daktari alisema nitakufa katika siku chache.” Amini tu.

“Alisema mtoto wangu hawezi kupona.” Lakini amini tu, hivyo tu. Amini tu kwamba Mungu alifanya ahadi.

163 “Kamwe sitatembea tena, Ndugu Branham, daktari aliniambia nisitembee.” Amini tu, kwa kuwa yote yanawezekana kwao waaminio. Amini tu, amini tu. Hivyo tu ndivyo inavyokupasa kufanya, amini tu, haidhuru. . . Halafu ilikuwa ni nini? Tayari amekufa. Vipi sasa? Kuamini tu. Hmm! Ninajisikia kubarikiwa sasa hivi, kweli najisikia. Loo, jamani! Amini tu!

“Ati amekufa?”

“Naam.”

164 Loo, ninakumbuka wakati alipokuja kwenye kaburi la Lazaro, “Kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa. Lakini hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa.” Jambo ndilo hilo.

165 “Mimi ndimi Ufufuo na Uzima,” asema Mungu. “Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi. Kila aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe. Unasadiki haya?”

166 Akasema, “Naam, Bwana.” Loo, napenda hilo. “Naam, Bwana, ninaamini Wewe ndiwe Kristo yule aliyekuwa aje ulimwenguni. Wewe ndiwe Mtiwa mafuta. Ninaamini kwa moyo wangu wote.”

Kasema, “Mmemzika wapi?” Amina.

167 Hakusema, “Nitashuka niende nione kile ninachoweza kufanya juu yake.” Loo, la. Loo, la. “Mmemzika wapi?”

168 Hakusema, “Yairo, vema, Yairo, samahani nilikuletea tatizo hili. Sasa, kanisa lako limekufukuza, nawe una shida na ndugu zako, na yote hayo, na—najua hilo,” na kadhalika. “Kweli nakuhurumia, Yairo, lakini, kama ningaliweza kufika huko mapema kidogo, mbona, huenda ingekuwa ni sawa, lakini, Yairo, na—na—nasikitika kukuletea tatizo hili.” Loo, la. Loo, la.

169 Alisema, “Je, sikukwambia, ‘Amini tu, ukitaka kuuona utukufu wa Mungu?’” Loo, nawazia hilo liliusaidia moyo wake, sivyo? Ninawazia nikiona maskini moyo wake ukiruka mapigo hayo, ukaanza tu kupiga kawaida tena.

170 Ndipo macho yake yakawa mbali na mzee wa wilaya, mbali na kuhani mkuu, mbali na kusanyiko lote. Huku akitembea huku na huku, akisema, “Utafanya nini kwenye kongamano lijalo, jamani? Utafanya nini?” Lakini alimkazia macho Yesu. Amina. Haya basi. Mwangalie Yesu, sijali yale mtu mwingine yeyote asemayo.

171 “Huyo jirani atasemaje?” Sijali jirani anasema nini. Hilo halina uhusiano wowote, ni yale Mungu aliyosema. Jirani siye hakimu wangu, Mungu ndiye Hakimu wangu, Yeye atanihukumu

kwa Yesu Kristo, ambaye ninamfuata. Amina. Haidhuru mtu mwingine yeyote anasema nini, ni Yale Mungu aliyosema, hayo ndiyo yanayolifanya kweli. Amina. Mungu alisema jambo hilo, linalifanya kweli. Wakosoaji wanaweza kusema chochote watakacho, lakini i—inahitaji Kile Mungu asemacho kukifanya kiwe ni kweli. Vema.

<sup>172</sup> Yesu alisema, “Amini tu.” Kuamini nini? Kuamini nini sasa? Amekufa! Amini kwa ajili ya *yasiyowezezana*. Amina. Sawa. Amini kwa yasiyowezezana. “Mbona, baada ya yeye kufa na kutiwa dawa asioze, niamini sasa?”

“Hakika, nilikwambia amini tu, unataka kuona utukufu wa Mungu.”

“Niamini nini?”

<sup>173</sup> “Amini chochote. Chochote. . . Amin, nawaambia, ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka,’ wala usione shaka moyoni mwako, amini tu, yatakuwa yako uliyosema.” Hiyo ni kweli.

<sup>174</sup> “Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi. Kila aniaminiye Mimi hatakufa kamwe. Mkikaa ndani Yangu na Neno Langu ndani yenu, ombeni mtakalo, nanyi mtapewa.” Hiyo ni kweli, ahadi hizi zote? “Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya, pia. Kazi kubwa kuliko hizi mtafanya, maana Mimi naenda kwa Baba Yangu.” Ahadi hizi zote hapa: “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Alijeruhiwa kwa makosa yetu,” *alijeruhiwa* kwa makosa yetu, “akachubuliwa kwa maovu yetu, adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, kwa kupigwa Kwake sisi *tuliponywa*.” Amini tu, amini tu.

<sup>175</sup> Anakuja hivi karibuni. Alimleta Ibrahimu, akamhesabia haki, akamtakasa, akamjaza na Roho Mtakatifu, akamweka kama mwana, akajionyesha Mwenyewe hai kwa kuugeuza mgongo Wake, na kuzungumza, akisema yale Sara aliyosema kwenye hema, kisha akabadilisha mwili wake, na kumtoa nje, akampa mwana.

<sup>176</sup> Amefanya jambo lile lile kupitia kwa Uzao wa Ibrahimu, yote ila kuabadilisha mwili, kuhesabiwa haki, kutakaswa, kujazwa na Roho Mtakatifu, kufanywa Mwana mwenye mamlaka, anakuja miongoni mwetu sasa, akijionyesha Mwenyewe kuwa hai, na kungojea kubadilishwa kwa mwili, Unyakuo upate kuja, utupeleke juu kumlaki Yeye. Hili hapa, kwa wakati wake tu. Amini tu. Endelea tu kusonga mbele. Ile saa kuu ya Mungu ya wakati inapiga vizuri kabisa. Loo, kwa ajili ya. . . Amini tu. Hakika.

<sup>177</sup> Kwa hiyo hatimaye Yesu anafika nyumbani, huku kila mtu akipaza sauti, “Ee, Bwana, Ee, Bwana, kwa nini ulifanya hivyo? Kwa nini ukafanya hivyo?”

Yesu anaingia kwa utulivu vivyo hivyo, kimya, kasema, “Tulieni, iweni na amani. Huyu msichana hajafa, amelala tu.”

Na, halafu, Biblia ilisema, wakamcheka.

Akasema, “Sasa, mnajua yeye ni nabii wa aina gani, wakati tumemia dawa asioze Naye anasema amelala.”

<sup>178</sup> Mngeweza kuwazia? Nayo Biblia ilisema, “Walimcheka kwa dhihaka,” wakimwaibisha, wakamcheka kwa dhihaka. Mnajua kile alichofanya walipolicheka Neno Lake? Aliwatoa nje. Na hivyo ndivyo hasa tutakavyofanya hatimaye.

<sup>179</sup> Nawe mkosoaji, hilo ndilo litakalokupata moja ya siku hizi, unalicheka Neno Lake, na kuzicheka kazi Zake, unasema, “Hao watu ni watakatifu wanaojibingirisha wanaonena kwa lugha na kucheza katika Roho.” Unasema wao ni kundi la watakatifu wanaojibingirisha, mnalicheka Neno Lake, kwa sababu hilo ni Neno lililofanyika mwili wa mwanadamu, hapa, likikaa miongoni mwetu.

<sup>180</sup> Baadhi yenu wahubiri huko nje, mnaosema hii ni telepathia ya kiakili, ama ibilisi, ama kitu kama hicho, siku moja itawabidi kughairi hilo Mbele Zake. Atawaweka nje ya Ufalme Wake kwa ajili yake. Hiyo ni kweli. Hatawaacha watu wamcheke, atawafukuza tena.

<sup>181</sup> Alipitia nyumbani na kulifukuza hilo kundi lote. Kila mtu aliyecheka, alitoka nje.

<sup>182</sup> Biblia ilisema, “Ukinena ninii moja...” Wakati Yesu aliposimama pale siku hiyo na—na alikuwa akipambanua roho, ndipo hilo kundi la makuhani likasema, “Mbona, huyo ni Beelzebuli, mpiga ramli,” mtu yeyote anajua mpiga ramli ni ibilisi, kwa hiyo akasema, “huyo ni Beelzebuli, mpiga ramli,” akiita kazi ya Mungu iliyokuwa ikiendelea, pepo mchafu, Yesu akasema, “Ninawasamehe hilo, lakini siku moja Roho Mtakatifu atakuja, ndipo ukinena neno moja dhidi Yake, hilo tu ndilo likupasalo kufanya, na kamwe hutasamehewa katika ulimwengu huu, na kwenye ule Ulimwengu mwingine utafukuzwa pia.” Hivyo ndivyo lilivyo zito. Mnaona? Naam, bwana.

<sup>183</sup> Hakuna msamaha wake katika ulimwengu huu, wala katika Ulimwengu ujao, kukufuru, ama kunena, ama kumwita Roho Mtakatifu kitu kichafu. Aliwatoa nje. Mnaona kinachotendeka leo? Jambo lile lile. Mnaona mahali wanapotokea, wakienda ulimwenguni, kiroho.

<sup>184</sup> Mnakumbuka pigo la mwisho lililoipiga Misri? Pigo la mwisho lililoipiga Misri lilikuwa ni lipi? ambalo lilikuwa ni mfano wa Kanisa likitoka. Lilikuwa ni mauti. Ni pigo gani la mwisho lililolipiga kanisa la Kipentekoste? Mauti ya kiroho. Linarudi nyuma moja kwa moja kama walimwengu wengine, mauti ya kiroho. Lakini wale waliotahiriwa, wakiwa na damu mlangoni, walipiga hatua za kurudi nyumbani, hiyo ni kweli kabisa, huku Nguzo ya Moto ikiwatangulia ili kuwaongoza.

<sup>185</sup> Loo, nina furaha sana usiku wa leo, nina furaha sana, usiku wa leo, kujua ya kwamba kuna tohara ya moyoni, kwamba Mungu atakatilia mbali ulimwengu wote, na mapokeo yote ya wanadamu, na chochote kile, nasi tunaweza kumwona Yesu, na kumwona amesimama pale katika Nguzo ya Moto, akitangulia, akizitenda kazi, na kufanya yale hasa Mungu alisema angefanya, na kuleta Kanisa lililojazwa na Roho Mtakatifu, na kufanya kazi, ambazo Yeye alisema. Nina furaha sana, usiku wa leo, kwamba hiyo ni . . . Mimi—mimi kabisa, mimi ndiye mtu mwenye furaha sana katika ulimwengu huu kwa sababu yake, kwa sababu Yeye aliahidi jambo hilo.

<sup>186</sup> Naam, Yeye aliwafukuza, kwa sababu walilicheka Neno. Naam. Ndipo akawatoa wote nje, halafu Yesu alikuwa peke yake na nini? Waliovunjika moyo, na waaminifu. Aliwaleta Petro, Yakobo, na Yohana: imani, tumaini, na upendo, akawaweka jengoni pamoja Naye, akawaweka hao wengine nje, basi Yesu alikuwa peke yake pamoja na waaminio waliovunjika moyo, wakilia kwa sababu walikuwa . . . msichana wao mdogo alikuwa amekufa amelala pale, maskini mtoto huyo alikuwa amelala, maiti, maua yamewekwa karibu naye. Kawaondoa wasioamini wote mbali Naye, namna hiyo.

<sup>187</sup> Loo, ni vigumu jinsi gani wakati kutokuamini! Kama vile jana usiku tulipokuwa tumeketi hapa mkutanoni, mchirizi huo wa kutokuamini ulipapiga mahali hapa, ulikuwa tu, palikuwa pabaya sana. Moja ya siku hizi usiku, nitashuka tu moja kwa moja na kuwaita jamaa hao watoke nje. Itaumiza hisia nyingi, lakini ni vema.

<sup>188</sup> Nilikuwa nikifanya hivyo wakati wote, nanyi mnajua nilifanya hivyo. Lakini ni—nimeshikilia, nimejizulia nayo, kwa sababu tu ya hisia za watu, maana ukiyang'oa ma—magugu, utapata ngano nyingi, pia. Mnaona? Kwa hiyo, sasa, wakati wa mwisho umekaribia sana sasa, kwa hiyo tutaendelea tu, tuendelea tu kusonga mbele. Lakini wakati . . . I—i—inapowazuia watu, kweli inawazuia watu wasioweza kuwa na imani, ambao hawawezi kuamini, mnaona, wakati kitu kama hicho kinapoendelea.

<sup>189</sup> Na kwa hiyo, ndipo alipotoa kila kitu, kila mtu ila tu imani Yake, tumaini, na upendo, wakisimama pale, Petro, Yakobo na Yohana, wale waaminifu, na baba halisi mwaminio, mama, Yeye aliiendea hiyo maiti. Loo! Mnaona?

<sup>190</sup> Asingeweza kufanya hivyo, huku amesimama pale, wote wakisema, “Mbona, angalia hilo? Ati *nabii*, naye anasema ati amelala. Sasa, niliwaambia, niliwaambia, niliwaambia. Mnaona jinsi ilivyo? Hilo—hilo . . . Hakuna kitu kwake. Kuna . . . ni lundo kubwa tu la mhemuko, kujichosha, hakuna lingine.”

<sup>191</sup> Yesu asingeweza kufanya lolote kulihusu, asingeweza kufanya lolote kulihusu usiku wa leo. Wakati alipokuja katika



nchi Yake Mwenyewe, si chochote, kazi nyingi angaliweza kufanya, kwa sababu ya kutokuamini kwao. Nao wakiendelea hivyo, wala asingeweza kufanya hivyo wakati huo, wala hawezi kufanya hivyo usiku wa leo. Lakini laiti angaliweza tu kuwafungia nje mahali ambapo angeweza kuwa pamoja na waaminio!

<sup>192</sup> Ndipo akaiendea ile maiti iliyokuwa imelala pale. Maskini msichana huyo alikuwa amekufa, labda ametiwa dawa asioze na amelazwa nje. Akamwendea na kumshika mkono, akaangalia huko nje kwenye ulimwengu wa anga, huko mbali mahali ambapo nafsi yake ilikuwa imeenda, na kusema, “Msichana, inuka.”

<sup>193</sup> Mauti yangewezaje kuwepo mbele ya Uzima? Maskini msichana huyo, makunyanzi kwenye paji la uso wake yakaanza, maskini paji lake la uso laini likaanza kukunjamana, kisha macho yake yakafunguka. Akamshika mkono, akamwinua, kasema, “Mpeni chakula. Wala msininii, kamwe msiseme lolote juu yake. Achaneni nao huko nje. Msiwaambie chochote, e—endeleni tu.” Mnaona? “Iacheni.”

<sup>194</sup> Loo, jamani! Mambo yote yanawezekana, amini tu. Yeye alikuwa nini? Alikuwa ni Neno la Mungu, mwili. Na, usiku wa leo, kuna . . . Mungu yeye yule ni ninii, Neno lile lile la Mungu liko katika mwili wako, ikiwa Kristo yuko humo ndani. Naye ni Bwana Yesu yeye yule, ungeweza kugusa vazi Lake, ama chochote utakacho. Kama utaamini tu kwamba Yeye yupo hapa, Yeye atakufanyia jambo lile lile. Unaamini hilo?

<sup>195</sup> Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu. Nitamwomba mpiga kinanda hapa, kama wataenda kwenye kinanda kwa muda kidogo tu. Ninawatakeni mpige *Amini Tu*.

<sup>196</sup> Kila mtu, sasa tafadhali msisogee huku na huku. Hebu kidogo tu. Baada ya kuhubiri namna hiyo, kwa namna fulani ni jambo gumu. Ninataka tu kuomba, nami ninataka kuona yale atakayofanya, niombe yale atakayonifanyia, niombe yale atakayowafanyia.

<sup>197</sup> Billy, aliniambia leo, yeye, ama, nilipokuja huko nje muda mfupi uliopita, nilipomleta mke wangu na hao wengine, alisema, “Baba, nilichelewa kidogo kule, nami nikavurugika, sikugawa kadi zozote za maombi.” Kasema, “Kwa nini usiwahubirie tu usiku wa leo?”

<sup>198</sup> Nikasema, “Sawa, nitafanya hivyo tu.” Kwa hiyo, lakini ninajisikia ya kwamba tutawaombea wagonjwa kwa vyovyote vile, kama tuna kadi za maombi ama hatuna. Mnaona? Tutawaombea wagonjwa kwa vyovyote vile.

<sup>199</sup> Ninaweza kumwona amesimama pale pamoja na Yairo. Ninaweza kumsikia yule tarishi akisema, “Usimsumbue, a—amekufa tayari. Mtoto wako amekufa, usi—usi—usisumbuke

tena. Matumaini yo—yote yamekwisha.” Na huko kuruka kwa pigo la moyo wa maskini mtu huyo!

<sup>200</sup> Labda, niliposema muda mfupi uliopita, sisi, hatutakuwa na mstari wa maombi, hatukusambaza wagonjwa wowote, kadi kwa ajili ya wagonjwa, huenda moyo wako uliruka, pia. “Nimekuja, Ndugu Branham, kuninii . . . Ni—ni—nilitaka kupata kadi ya maombi usiku wa leo, ninataka kuombewa.” Amini tu. Kama ukininii tu—ukiamini tu, hivyo tu. Tayari amesema Neno, amini tu. Haikubidi kupanda hapa juu, kaa tu mahali ulipo na uamini tu, kwa kuwa Yeye alisema, “Mambo yote yanawezekana, amini tu.”

<sup>201</sup> Ninawatakeni mwe na kicho kabisa. Ombeni tu sasa. Kila mgonjwa humu ndani, kila mtu humu ndani aliye mgonjwa na anayetaka Kristo aje kwako, ninakutaka uinue mkono wako. Inua tu mkono wako popote ulipo, mtu mgonjwa humu ndani. Vema. Kila mahali tu, karibu wote.

<sup>202</sup> Kwa sasa, wekeni mikono yenu chini. Sasa, maskini mwanamke huyo alifanya nini? Aligusa vazi Lake. Alishuka kule amechelewa sana kupata kadi ya maombi, tungesema. Lakini aligusa vazi Lake. Alipata uponyaji wake, kama tu vile roho ya maskini yule msichana mdogo ilivyovutwa ikarudishwa, kama Yeye alimwekea mikono, ama kama msichana alimgusa, ama—ama, wote wawili walikuwa ni Wayahudi, kwa hiyo kama alimgusa Yeye, ama, yule msichana aliyekufa asingeweza kungusa, kwa hiyo ilimbidi Yeye kungusa yule msichana aliyekufa. Kwa hiyo unaweza kungusa usiku wa leo, Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.

<sup>203</sup> Ninyi huko nje kwenye kusanyiko, nyote hatufahamiani. Ninamwona Ndugu Ed Daulton ameketi *hapa*. Nami najua nina marafiki wengine. Mimi . . . Loo, *hapa* pembeni wameketi jamaa fulani kutoka Tennessee, ndiyo kwanza nikutane na yule msichana mdogo hapa nje ukumbini akiingia.

<sup>204</sup> Sasa nitasema hivi: Endapo wewe ni asiyeamini, hata nisingekaa humu jengoni, ama karibu na hili jengo. Kwa sababu ninataka kuwaambia, ya kwamba kama pepo wachafu, kama kansa au kadhalika, wangeondoka . . . Nasi sote tunajua wao ni uhai, maana wako ndani yetu wakiyaangamiza maisha yetu. Basi kumbukeni, katika Biblia wakati hao pepo wachafu walipotoka kwa mmoja, waliingia kwa mwingine. Kwa hiyo kama wewe si mwaminio, nisingekuwa karibu sasa, maana kuna waaminio walio karibu. Basi kumbukeni, ni mara ngapi nimewaapisha, ni mara ngapi nimewaonyesha, kwamba mambo hayo mfanye? Baada ya mkutano kwisha, karibu kila mara kuna mtu anayepiga simu, ama kuandika, “Ndugu Branham, ni—ni—nilikuwa asiyeamini, nami nilienda hivi majuzi, wakati mwanamke yule, uliyemwambia alikuwa na kansa, nikasema, ‘Huo ni upuuzi,’ ndipo daktari akaniambia nina kansa sasa.”

Mnaona? Mnaona? Kumbukeni tu. Ninanena katika Jina la Bwana Yesu. Ni juu yako, ni juu yako.

Sasa, iweni tu na imani na mwamini.

<sup>205</sup> Baba yetu uliye Mbinguni, Jina Lako Litukuzwe. Ufalme Wako uje. Mapeenzi Yako yafanyike duniani, kama huko Mbinguni.

<sup>206</sup> Mungu wa milele na mwenye Neema, ninaomba usiku wa leo, ya kwamba Wewe katika kusanyiko hili...Ninapenda tu kuzungumza juu Yako, Yesu. Wewe ni...Umekuwa maisha yangu kwa miaka thelathini na mmoja. Jinsi ninavyokupenda! Jinsi, nina furaha sana kwamba usiku huo, kwamba ni—nilikukubali Wewe kama Mwokozi wangu! Nina furaha sana, nina furaha sana kwamba uliponiagiza kwenda kuihubiri Injili, na halafu usiku huo uliponiambia, “Nenda, ukawaombe wagonjwa,” na kuniambia ya kwamba hayo maono yaliyokuwa yakija, hayakuwa kile ndugu zangu walichokuwa wameniambia kilikuwa ni pepo mchafu, bali ilikuwa ni Wewe, nayo yangelichochea taifa zima, ulimwengu mzima katika uamsho, na yamefanya hivyo, Bwana. Maneno Yako ni kweli.

<sup>207</sup> Na ndipo uliposimama pale, juu yangu, siku ile huko chini mtoni, wakati hao maelfu ya watu wakisimama pale wakiangalia, moja kwa moja kwenye saa nane alasiri, kutoka kwenye anga hizo za shaba, na Nuru ile kubwa ikinguruma kote juu, ile Sauti ikisema, “Kama vile Yohana Mbatizaji alivyotumwa, Ujumbe huu utakuwa ni wa Pili, kabla ya kuja kwa Kristo,” nasi tunaona, Bwana, umefanya jambo lilo hilo, nasi tunaona wakati ukisonga mbele sasa. Maneno Yako yote ni ya kweli. Na sasa, sisi hapa mwishoni mwa safari, moja kwa moja nje, tukiokota masazo kwenye mashamba hapa, tukiokota nyasi za mwisho kutoka kwenye uamsho huu wa mwisho.

<sup>208</sup> Sasa, Baba, tuko mara nyingine tena, tena, katika njia panda hizi kuu za ulimwengu hapa, usiku wa leo, Chicago, Illinois. Jinsi watu wametamani kusema, “Loo, laiti ingeweza kutikiswa, kama ingeweza kutikiswa!” Ee Mungu, hicho chakula cha atomiki kinachoenda mbio huko nje mtaani hakitikiswa kamwe; kitatikiswa kwa bomu la atomiki. Lakini Kanisa Lako limetikiswa kuliko wakati mwingine wowote, limeona mambo ambayo halijawahi kuona, wala hakuna kanisa nyuma yake lililo yaona, tangu Kristo alipokuwa duniani. Limetikiswa, Bwana, watu Wako halisi wameamini kwa moyo wao wote.

<sup>209</sup> Sasa, wakati wa badiliko umewadia, ukame mkuu, ukame wa kiroho kuikumba nchi, na halafu Kuja kwa Kristo. Ninaomba ya kwamba utatujalia, Bwana, usiku wa leo, ya kwamba wakati huu mwingine tena, ili kwamba Injili...

<sup>210</sup> Na labda huenda kukawa na mgeni miongoni mwetu. Kama mtu huyo yuko hapa usiku wa leo, na ametoka chini ya ile Damu, naomba, Mungu kwamba jambo fulani litafanywa, kwamba

utafanya jambo fulani usiku wa leo, kama ulivyofanya huko chini Emau, wakati huo, na kuthibitisha ishara kwa watu, kama tu ulivyofanya kabla ya kusulubiwa Kwako, wapate kujua ya kwamba Wewe ni Yesu yeye yule aliyefufuka katika wafu, na yupo hapa usiku wa leo.

<sup>211</sup> Ninajikabidhi mwenyewe pamoja na ujumbe uliotangazwa, na Kristo aliyepo, kwa Mwenyezi Mungu, huduma Yake ipate kuendelea. Katika Jina la Yesu, wengi na wasaidike. Amina.

<sup>212</sup> Sasa, katika Jina la Yesu Kristo, ninachukua kila roho humu ndani chini ya mamlaka yangu, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Sasa, iweni waaminifu, ombeni. Iweni tu na imani.

<sup>213</sup> Sasa, hatutaita kadi za maombi hapa juu, maana sidhani tuna zozote hapa ndani, huenda kukawa na msukumano mara kwa mara. Muda umeenda sana kwa vyovyote vile, kufanyiza mstari wa maombi, wakati umepita, ni saa nne sasa. Lakini nataka kusema jambo fulani, ninyi watu wote huko nje mnaojua ya kwamba hatufahamiani, nawe ni mgonjwa, na unaamini ya kwamba Kristo ni Kuhani Mkuu, kwamba Yeye alinituma hapa kuwa tu ni M—Mzabibu, ninamaanisha tawi kwenye Mzabibu, unaamini ya kwamba kama ungeweza kumgusa Yeye, Yeye angenena kupitia kwangu na kufanya kazi ile ile, inua mkono wako, unajua ya kwamba sikujui. Asanteni.

<sup>214</sup> Sasa, angalieni huku. Kisa kimoja kinapaswa kulithibitisha, lakini hebu na tupate angalau vitatu. Ninawatakeni mwamini kwa moyo wenu wote. “Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana.”

<sup>215</sup> Sininii... Unasema, “Nianze upande gani, Ndugu?” Sijui, ni kwamba Yeye anaanzia upande gani, mahali atakapoanzia, ninaweza tu kwenda aendavyo. Mnaona? Inanibidi tu kuangalia, na popote inapoanzia, ninaangalia ki—kitu fulani, ni kutiwa mafuta. Sasa, mimi hapa, Mungu anajua. Mnaona? Lakini mbele ya Neno Lake kwamba si—siwajui. Ninajua watu wawili au watatu, mmoja aliyeketi papa *hapa*, ama wawili. Nafikiri huyo ni Dada Downing, hiyo ni kweli? Nafikiri ndivyo. Mnaona? Ninamjua mtu huyu aliyeketi *hapa*, Ndugu yangu na Dada Dauch *pale* pembeni, wawili wameketi *pale*.

<sup>216</sup> Nitajaribu kuwapa kisogo. Hata kama... Ingenibidi kuninii... Kama akija juu yao, intanibidi kusema pale, kwa sababu hilo tu ndilo ninaloweza kusema. Ni wangapi wanaoamini, kabla jambo lolote halijatukia, mnaamini ni kweli? Mungu awabariki.

Unaona hilo, Shetani? Wewe ni mwongo!

<sup>217</sup> Unasema, “Je, anakujaribu hivyo, Ndugu Branham?” Mbona, bila shaka yeye husimama, anajaribu kunijaribu. Kama anakujaribu wewe, unafikiri ananifanyia nini, hapa?

218 Kuna mtu ameketi papo hapo nyuma, anayemwombea mtoto, aliyeketi hapo karibu, ana tatizo miguuni mwake. Hiyo ni kweli, sivyo? Sikujui, hatufahamiani. Lakini, Bw. Farmer, unaamini ya kwamba Mungu atamponya huyo mtoto na kumpa afya? Endapo hatufahamiani, inua mikono yako namna *hiyo*. Je, hilo ndilo ulilokuwa ukiombea? Je, hilo ndilo jina lako na yote kulihusu? Inua tu mkono wako. Umepata haja yako.

219 Yupo mama aliyeketi papa hapa. Ana yabisi kavu, ana ukurutu sikioni mwake. Bibi McGill, simama kwa miguu yako kama hiyo ni kweli. Kama hatufahamiani nawe, pungu mkono wako. Punga mkono wako endapo mimi...hatufahamiani. Umepata haja yako. Nenda nyumbani, Kristo amekuponya.

Mbele za Mwenyezi Mungu, sijawahi kuwaona watu hao maishani mwangu. Ninawaomba mwamini. Iweni tu na imani, msiwe na shaka.

220 Huku nyuma kabisa, mwishoni mwa safu, nyuma kabisa kuelekea upande wa nyuma, mama aliyeketi pale ana ugonjwa wa mapafu, ana wasiwasi juu yake. Mungu, nisaidie kumjua. Bibi Miller, simama na ukubali uponyaji wako, Yesu Kristo anakuponya. Kama huyo ni wewe, nami ni mgeni kwako... Je, una kadi ya maombi, Bibi Miller? Huna? Huhitaji moja. Vema. Nenda nyumbani, uwe mzima, Yesu Kristo anakuponya.

221 Huyo mama, mama mweusi, aliyeketi moja kwa moja nyuma yake, moja kwa huko nyuma kwenye...huku kutoka kwangu, ana u—uvimbe, unajiandaa kwenda hospitalini kufanyiwa upasuaji, ama wanakutaka uende. Maskini mama, ninaweza tu kumwona katikati ya wazungu wawili. Simama, mama. Hatufahamiani, sikujui. Una kadi ya maombi? Huna. Sijawahi kukutana nawe maishani mwangu. Hatufahamiani. Kama hiyo ni kweli, pungu mkono wako *hivi*. Nilichokuambia ni kweli? Yesu Kristo anakuponya. Nenda nyumbani ukapokee uponyaji wako.

Mnaamini?

222 Hapa, angalieni huyo roho wa pepo, huyu hapa akija moja kwa moja upande huu, giza hilo linaingia moja kwa moja juu ya mwanamke huyu hapa, mwanamke mwingine mweusi aliyeketi papa hapa. Una kadi ya maombi, mama? Huna. Huhitaji moja. Wewe pia una uvimbe. Unataka nikwambie ulipo? Uko kwenye bega lako la kushoto, chini ubavuni mwako na nyongani. Hiyo ni kweli, sivyo? Amini kwa moyo wako wote.

223 Bibi Holtzmaster, huko nyuma akilia, unafikiri una kansa, lakini uta—utakuwa sawa. Mungu akubariki. Simama. Sikujui. Unaogopa kansa, sivyo? Lakini ilikuacha, ni sawa.


224 Aisee, utanipa fadhila, Dada, ambapo Mungu amekupa moja? Hatufahamiani, sivyo? Weka mkono wako juu ya mwanamke huyo nyuma yako, mwite Bibi McAllister, yeye hanijui, McAllen, hasa. Ana shida ya kichwa chake, lakini

itamwacha, naye atakuwa sawa. Hasikii vizuri sana. Vema. Yote yamekwisha sasa, Bibi McAllen, unaweza kwenda nyumbani pia. Unaamini Yesu Kristo sasa anakuponya? Vema. Basi nenda nyumbani, ukaponywe.

<sup>225</sup> Ni wangapi wanaomwamini sasa, kwamba Yeye ni Yesu Kristo? Ni wakati wa kujitokeza jukwaani. Ni wakati wa kuamini kwa moyo wako wote. Unaamini hilo? Ni wangapi watamkubali sasa kama Mponyaji wenu? Amevuka jengo, huku na huko, ndani na nje, mbele na nyuma, mkiliamini. Mnaamini kwa imani yenu yote—imani yenu yote mwezayo? Simameni kwa miguu yenu katika Jina la Yesu Kristo na mpokee uponyaji wenu. Inueni mikono yenu.

<sup>226</sup> Rudieni nyuma yangu: “Bwana, naamini, ya kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu. Ninakataa kutokuamini kwangu. Ninakukubali kama Mwokozi wangu, ninakukubali kama Mponyaji wangu, ninakukubali kama Mfalme wangu. Ninakuamini Wewe sasa Bwana, tangu sasa, ushuhuda wangu hautakuwa hasi, nitakusifu, katika Jina la Yesu Kristo.”

Sasa, inueni mikono yenu mkamsifu, na yote yamekwisha.

<sup>227</sup> Mungu awabariki, ninawakabidhi kwa mzee. 

61-0427 Amini Tu  
Stephen Mather High School  
Chicago, Illinois Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

[www.branham.org](http://www.branham.org)